

Huyu Melkizedeki Ni Nani?

Jeffersonville, Indiana, USA

Februari 21, 1965J

1 Na tuinamishe vichwa vyetu kwa maombi.

Mpendwa Baba wa Mbinguni, tunasikia wimbo huu wa *Amini Tu*, unatufanya tujue ya kwamba hayo tu ndiyo tunayopaswa kufanya kurithi yo yote ya ahadi za Mungu, kuziamini tu. Kwa maana imeandikwa, "Mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio." Tunapolia, kama yule mtu aliyekuwa na mtoto mwenye kifafa, "Bwana, ninaamini! Nisaidie kutokuamini kwangu."

Tunakushukuru kwa uweza wako mkuu, kule kujifunua Kwako kuu kwa ajili yetu katika siku hizi za mwisho. Inaifanya mioyo yetu iwe na furaha na shangwe kujua ya kwamba tumeunganishwa na Mungu aliye Hai; Ambaye hujithibitisha katika mwili, ushahidi wa vitu, kama alivyofanya siku zilizopita na kama alivyoahidi kwa ajili ya siku hii. Tunakushukuru sana Wewe, Mungu wetu. Katika siku hizi zenye giza ambapo yaonekana hamna mtu anayejua ataiendea njia ipi, tunashukuru sana ya kwamba tulipata mahali salama, kimbilio.

Sasa tubariki usiku wa leo, Bwana, tunaponena juu ya Neno Lako. Na ahadi ambazo tumepewa, na tuzitunze mioyoni mwetu, tukazilinde kwa kicho, na tukazizingatie kwa nidhamu halisi ya uungu. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

2 [Mtu fulani anazungumza na Ndugu Branham — Mh.] Sadaka ya upendo? Hawapaswi. Hawapaswi kufanya hivyo. Ni nani aliyefanya hivyo? Una hatia? Nilikuwa nikimkemea msimamizi. Akasema alichukua sadaka ya upendo kwa ajili yangu. Hapaswi kufanya hivyo. Ninathamini jambo hilo, Mungu anajua jambo hilo, bali si—sikuja kwa ajili ya jambo hilo. Asanteni. Bwana na awabariki. Nitafanya kila niwezalo. Nitaiweka moja kwa moja kwenye umishenari wang'ambo, ndivyo nitakavyojua ya kwamba itatumiwa kwa ufalme wa Mungu. Na Bwana akipenda, nitaichukua mwenyewe kwenda ng'ambo kuleta Injili ile ile ambayo mmekua mkiketeki, mkiisikiza juma hili ndipo nitajua itatendwa kama mliyovamini. Bwana anisaidie kufanya jambo hilo.

Ninashukuru sana kwa ajili ya mahudhurio makubwa ya juma hili, na kwa ninyi watu wote mliounganishwa usiku wa leo tena na—na nyaya za simu. Nasi tunashukuru kwa kila mmoja wenu.

3 Billy aliniambia asubuhi ya leo, akasema, "Baba, kama ungalikuja nami asubuhi ya leo, alfajiri, baada tu ya mapambazuko, na kusimama nje mahali hapa na kuona kina mama wakiwalisha watoto wao motokaani, maskini watu hao wakiketeki katika mvua wakingojea milango ifunguliwe" Mnaona namna ningekuwa mnafiki kama ningewaambia lo lote ila Kweli? Kwa kweli ningekuwa mtu mchafu. Wakati mwingine inanibidi kuumiza, lakini si kwa sababu ninataka, ni kwa sababu ... Si mimi ninayeumiza. Ni Kweli inayoumiza. Nami ni—ni ... Lakini ninaamini hiyo ndiyo sababu ya wewe kuja, kwa sababu mimi ni mwaminifu sana kwako, na kufanya yote niwezayo kukusaidia. Bwana na amsaidie kila mmoja wenu.

4 Na sasa, nataka kuwashukuru watu kwa ushirikiano wao mzuri, wenyeji wa mji huu pia, waliotupa—wakaturuhusu hili—kukodisha jumba hili la shule, jumba la mikutano, pamoja na jumba hili la michezo. Nami nataka kuwashukuru viongozi kama mko hapa. Na pia ninataka kumshukuru Thurston Colvin, ambaye ndiye msimamizi hapa, kwa ushirikiano wake mzuri katika kutusaidia kupata hili na kuwa pamoja nasi kila usiku.

Tunalishukuru jeshi la polisi la Jeffersonville kwa kuja hapa na kuangalia, kwa gharama nafuu sana. Nafikiri yapata dola mbili kwa saa, kwamba polisi waliwekwa hapa kwenye jukumu maalum, kuegesha magari, kuona ya kwamba hakuna ... hakuna kitu kilichotendeka, na kila kitu kilikuwa sawa. Tunawashukuru watu kwa ajili ya jambo hilo. Na kwa—kwa, pia, mhandisi hapa kwenye—kwenye ubao, nimemwona. Na wote wanaohusika na jambo hili, hakika tunawashukuru.

5 Ninamshukuru kila mmoja wenu kwa ajili ya karama hizi. Billy ameniletea tu aduhuri ya leo za—zawadi, zawadi nyingi katika vijisanduku, peremende na vinginevyo. Na moja yazo ilikuwa zile—zile safu za Heri pamoja na picha ya Kristo iliyochorwa hu—humo, Ilikuwa yale mahubiri mlimani. Na hakika ilikuwa nzuri. Hakika ninawashukuru. Na mambo mengi sana, sijui jinsi ya kuwashukuru kwa ajili yake. Ndiposa, pia kwa—kwa kudhaminia, kugharimia mikutano hii, bila shaka tunawashukuru kwa mioyo yetu yote. Bwana ambariki kila mmoja wenu, sana.

Billy alisema, kulikuwako na watu wengi, mlikuwa mkiomba mahojiano ya kibinafsi wakati huo. Na wengi waliomba na walikuwa na watoto wadogo wa kuwekwa wakfu. Loo, namna ninavyotaka kufanya jambo hilo!

Lakini, mnaona, nitakapokuja wakati huu, ni jambo la haraka sana. Sina budi kukaa sawa, wakati wote, katika kusoma, Neno hili na maombi, kwa sababu ya kuleta Jumbe hizi. Mnaona, wao si ... Wao—wao ni wa ajabu sana kwetu, kwa sababu ni kupata mapenzi ya Mungu na kisha kunena mambo hayo. Na hayo yote hayana budi kuungana pamoja, na kumuuliza Mungu ni lipi hasa litafunguliwa.

6 Sasa, Bwana akipenda, tutarudi tena hivi karibuni, mara tu tutakapopata siku. Nilitoa sha—sha, ama—ama nilisema jambo fulani kuhusu Pasaka. Afadhali niangalie hilo, kwa sababu nafikiri nina ratiba huko California karibu wakati huo. Kwa hiyo hilo huenda likawa ni kosa. Hata hivyo, tutakaporudi tena kwenye Maskani, tutawatamia kadi, na kanisa, na—na kuwapa—tarehe na wakati. Ndipo basi, labda wakati huo, tena ...

Sijaweka wakati wowote wa kuwaombea wagonjwa. Hatujapata kuwa na ibada moja ambayo tuliwaleta watu na kuwaombea. Tumekuwa tukiwatuma. Na ndugu zetu hapa wamekuwa wakihubiri, Ndugu Lee Vayle na Ndugu ... Hawa ndugu wengine wamekuwa wakihubiri, na kuwaombea wagonjwa, na kufanya ubatizo wa maji, kubatiza, hasa, na kuniruhusu nikae peke yangu na Neno. Tunawashukuru watu hawa. Walifanya kazi ya kishujaa.

7 Kuna marafiki wengi sana hapa ningetaka kukutana nao. Ninaangalia chini na kumwona John na Earl. Na kuna Daktari Lee Vayle, mmoja wa wasimamizi wa kampeni. Ndugu Roy Borders. Hao watu, hata sina ... Sina hata zaidi ya kuwapa mkono. Sijapata nafasi ya kufanya hivyo. Ninawazia juu ya marafiki zangu kutoka Kentucky, na kila mahali hapa, na marafiki wahudumu, namna ambavyo ningetaka kuwapa mikono! Ndugu Blair, nilimwona hapa hivi majuzi. Na wengi wa hao watu ambao ni—ninawapenda, nao wamehudhuria mikutano kadha, wala sijapata hata kuwapa mkono. Ni—ninajaribu ... Si kwa sababu sitaki kufanya hivyo; ni kwa sababu sina wakati wa kufanya jambo hilo, nami nina haraka tu.

8 Kuwaweka wakfu watoto wachanga, hakika. Mwanangu mwenyewe, mjukuu wangu mdogo alipaswa kuweka wakfu kwenye mkutano huu. Sijapata wakati wa kufanya jambo hilo; mtoto Daudi. Mimi ni babu, mara mbili sasa. Kwa hivyo Bw. May, iwapo yuko hapa usiku wa leo, aliyenipa ile fimbo, inaonekana sina budi kuitumia hivi karibuni.

Nami nilimwambia Billy, nikasema, "Biblia bila shaka ilisema mkaongezeke, mkajaze nchi, bali mzigo huo wote haukupewa wewe." Na wajukuu hawa wanaonekana upesi.

Na sasa kumbukeni, mkwe wangu alikuwa tasa kwanza; hangaliweza kupata watoto. Asingeweza kuwa na watoto. Na siku moja, tukitoka kwenye mkutano, Bwana alinena nami na kusema, "Loyce, utazaa mwana. Bwana amekubariki. Shida yako ya kike imeisha." Mtoto Paulo alizaliwa, miezi tisa baadaye.

9 Miezi miwili kabla mtoto huyu hajatokea, nilikuwa nimeketi, nikila kiamshakinywa asubuhi moja, mezani, na Loyce na Billy walikuwa wameketi upande wa pili wa meza kutoka kwangu. Nami nikamwona Loyce akimlisha mtoto mchanga kwa pinki ... ama blanketi ya bluu iliyomzunguka. Naye Billy alikuwa ameketi pembeni, akimlisha mtoto Paul. Nikasema, "Billy, niliona tu ono. Loyce alikuwa akimlisha mtoto mchanga aliyevikwa blanketi ya bluu."

Akasema, "Hiyo ndiyo safari yangu ya kuwinda. Hiyo ni miezi tisa tu tangu sasa."

Miezi kumi na moja baadaye, mtoto Daudi alizaliwa. Nami sijaweza kumweka wakfu kwa Bwana bado, na hatutafanya hivyo mpaka tutakaporudi tena. Kwa hiyo mnaona ni kitu gani.

10 Namna ninavyowapenda watu na ushirika wao! Lakini ndugu zetu wamekuwa wakiwaombea wagonjwa, nami najua limefanikiwa. Kila usiku tuliwaombea wagonjwa, mmoja akiweka mikono yao juu ya mwingine, sisi sote pamoja, ambayo kwa njia hiyo inashikilia upeo wote. Lakini labda, Mungu akipenda ... Nitaiweka kwenye kadi, kama tukituma. Nikirudi, ningetaka kutenga siku mbili tatu tena kuomba tu wagojwa na kufanya tuwezavyo hivyo. Sasa, nami nawashukuru watu kwa msaada wao, tena.

11 Sasa nataka tu kutoa maoni, kwa muda kidogo tu, juu ya—juu ya Ujumbe wa asubuhi. Bila shaka, sikuomaliza kabisa, bali nafikiri mnaelewa. Nami nina hakika hamkuninii ... Hamtajua kamwe hiyo ilikuwa nini kwangu kutenda.

Sasa, inaonekana ni rahisi sana kwenu. Lakini, wewe, unaona kile unachofanya? Unachukua mahali pa Mungu, kutamka kitu Fulani. Na kabla sijafanya jambo hilo, ilibidi lije jibu kutoka kwa Mungu. Naye ilimbidi ashuke, Naye alijionyesha Mwenyewe dhahiri, na kutoa Ufunuo. Kwa hiyo, mnaona, hili ni kwa Kanisa. Na kumbuka, nilisema, "Haya, haya niliyosema, yalikuwa kwa ajili ya Kanisa pekee."

Na ili mkapate matumaini na kujua, huyo alikuwa Mungu yule aliyeniambia kule ambako hakukuweko kuchakulo wo wote. "Nena, na useme watakapokuwa." Na ilitokea mara tatu mfululizo. Naam, kama yeye anaweza kwa Neno lilo hilo kuumba kitu kisichokuwepo, ni zaidi vipi hili litasimama imara kwenye ile siku ya hukumu! Mnaona? Watu walikuwa pale kuona mambo haya, na kujua. Kama vile Paulo alivyosema, katika siku zilizopita. Kuna watu waliokuwa pamoja naye ambao—waliosikia nchi ikitetemeka na hawakuisikia ile sauti, bali wao—waliona ile—ile Nguzo ya moto.

12 Ilinifurahisha ingawaje baada ya kuomaliza kuona mabwana na wake zao ambao najua ni Wakristo halisi wakikumbatiana wao kwa wao na kulia.

Na sikizeni, marafiki Mungu huthibitisha Neno lake kwa ishara na ushuhuda kuhakikisha ya kwamba ni kweli. Sasa kumbuka, ile Nuru iliyokuwa katika Wingu hilo, iliyotoa Ufunuo. Nilikuwa ...

Msichana wangu mdogo alikuwa akiniambia, Sara hapa, ya kwamba wakati wao ... Ile shule pale Arizona ilikuwa ikitazama kule juu kwenye anga zisizo na mawingu na kuona wingu hili la ajabu, kule mlimani, likienda juu-chini pamoja na moto wa majano uliowaka mle ndani. Mwalimu aliachilia madarasa na shule, na kuwaleta mbele, na kusema, "Je! Ulipata kuona kitu kama hicho? Angalieni huko."

Kumbukeni, hiyo ndiyo nuru ile ile manjano iliyo kwenye ule mwamba! Kwa hiyo ni Mungu yeye yule, Ufunuo ule ule, uliosema, "Waambie wafanye *hivi*." Ndivyo nilivyowaambia asubuhi ya leo, kwa hiyo ndiyo ilivyo.

13 Kama ikitokea kwamba rafiki yangu mzuri, Ndugu Roy Roberson, anasikiliza huko Tucson. Roy, unakumbuka, hivi majuzi, ono uliloona tulipokuwa tumesimama juu ya mlima? Ulinijia, na hilo Wingu lilikuwa juu ya kilele? Ukashuka, unajua Yeye alivyokwambia, si nilikwambia mle nyumbani hivi majuzi? Ndiyo hiyo, Roy. Usijali tena, mwanangu. Imekwisha.

Hujui hilo linamaanisha nini! Ni neema. Yeye anakupenda. Nanyi mnampenda, mtumikieni Yeye kwa unyenyekevu na kumwabudu siku zenu zilizosalia. Furahini, endeleeni kuishi mnavyoishi. Kama mna furaha, endeleeni hivyo. Msifanye kosa lo lote tena, namna hiyo. Endeleeni tu. Ni neema ya Mungu.

14 Sasa nataka kuomba tena kabla hatujaingia katika Neno. Ni wangapi wataniombea? Ninaenda tu kutoka mkutano hadi mkutano. Mtaniombea?

Mnajua, ningetaka kuwambia wimbo mdogo, sisi sote pamoja, kabla hatujaenda kwenye Neno. Ili tu ... kusudi tumjue Mungu ... Kujitolea tu kidogo. Je! Ulipata kusikia wimbo huu mdogo, *Yeye Anakujali?* "Kupitia mwangaza wa jua na huzuni, Yeye anakutunza."

Bibi mdogo anakuja kwenye kinanda. Aisee, ninataka kumshukuru mama huyu mdogo, pia. Hata sikujua alikuwa ni nani. Ni mmoja wa binti za shemasi hapa. Hakika mimi ... Msichana mdogo wa Ndugu Wheeler. Yeye amekua sasa. Alikuwa ni mtoto mdogo aliyekaa kwenye goti langu, si muda mrefu uliopita, na sasa yeye ni msichana. Kwa hiyo kwa kweli ninamshukuru kwamba ametumia kipaji chake katika muziki, na sasa anacheza vizuri sana. Waweza kutupa sauti, dada? Sisi sote pamoja sasa.

Yeye anakujali,
Yeye anakujali;
Mwangani ama kivulini,
Yeye anakujali.

Mnapenda jambo hilo? Hebu na tuimbe tena, sote pamoja.

Yeye anakujali,
Yeye anakujali;
Mwangaza au kivulini,
Yeye anakujali.

Ndugu Dauch, Yeye hukutendea hayo pia, Ndugu. Hivi hamumpendi? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

15 Mungu mwenye neema, kwa haya maandishi mdogo ya mambo machache ya kuwaambia watu na kurudi tena kutaja tena asubuhi ya leo, kwa maana hayo ndiyo watu huja kusikia. Ninaomba, Mungu, ya kwamba utawaruhusu watu waone ya kwamba Mungu anapenda na kujali. Na si mimi niliyetoa hayo Bwana, ilithibitishwa ya kwamba ilikuwa kweli. Kwa hiyo ninaomba, Mungu Mpendwa, ya kwamba upendo Wako daima utadumu miongoni mwa watu. Usiku huu, tutahitsjika kutengana baada ya mkutano huu na kwenda kwenye nyumba zetu mbalimbali, hilo—hilo kwa namna fulani linstursrus, baadhi, mno, Bwana. Ninaomba ya kwamba utawabariki watu hawa.

Sasa tunapokaribia Neno, katika maombi, na kulikaribia Neno lililoandikwa, tunaomba ya kwamba utalichukua Neno hili lililoandikwa na kulifanya hai kwetu usiku wa leo. Na tunapoondoka kwenye hili jengo kuachana kwenda nyumbani mwetu mbali mbali, na tuseme kama wale waliokuja toka Emau, waliokuwa wametembea Naye siku nzima na bado hawakumjua...bali alipowaingiza mle chumbani usiku huo, huku milango yote imefungwa, Yeye alitenda jambo fulani jinsi alivyotenda kabla ya kule kusulubishwa Kwake. Kwa jambo hilo, walijua alikuwa amefufuka tena.

Fanya hivyo tena usiku wa leo, Bwana. Tujalie, wakati milango imefungwa, na kundi Lako dogo hapa limeketi, likingojea. Na, Baba, tunapoenda nyumbani mwetu, tutasema kama walivyosema, "Je! Mioyo yetu haikuwaka ndani yetu alipokuwa akisema nasi njiani!" Tunajiweka wenyewe, na wote, mikononi Mwako, Bwana. Fanya nasi kadiri utakavyo. Katika Jina la Yesu. Amina.

16 Sasa hebu na tuingie kwenye ibada sasa, upesi. Mkifungua sasa pamoja nami, mkipenda, kwenye Kitabu cha Waebrania, na ufunuo mwingine juu ya Ujumbe. Tutazungumza kwa muda mchache tu usiku wa leo, Bwana akipenda. Na halafu tunaposoma vifungu vitatu vya kwanza vya Waebrania 7:1 hadi 3, na kisha kutoa maoni juu ya jambo hili. Nasi hatujui Bwana atafanya nini; hatujui. Jambo pekee tunalofanya ni kuamini tu, kukesha, kuomba. Hiyo ni kweli? Na amini ya kwamba Yeye atafanya mambo yote yafanye kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema kwa sababu aliahidi kufanya hivyo.

Kwa maana Melkizedeki huyo, mfalme wa Salemu, kuhani wa Mungu aliye juu, aliyekutana na Ibrahimu alipokuwa akirudi katika kuwapiga hao wafalme, akambariki;

Ambaye Ibrahimu alimgawia sehemu ya kumi ya vitu vyote; (tafsiri ya jina lake kwanza ni mfalme wa haki, tena, mfalme wa Salemu, maana yake, mfalme wa amani;

Hebu na tusome mbele kidogo.

Hana baba, hana mama, hana wazazi, ... hana mwanzo wa siku zake, wala mwisho wa uhai wake, bali amefananishwa na Mwana wa Mungu); huyo adumu kuhani milele.

17 Wazia juu ya Mtu huyu mkuu, jinsi Mtu huyu alivyo mkuu! Na sasa, swali ni, "Mtu huyu ni nani?" Wanatheolojia wamekuwa na mawazo mbalimbali. Lakini tangu kufunguliwa kwa ile Mihuri Saba, kile Kitabu cha siri ambacho kimekuwa cha siri kwetu ... Kulingana na Ufunuo 10:1 hadi 7, siri zote zilizoandikwa katika Kitabu hiki, ambazo zimefichwa kote katika wakati wa watengenezaji, zinapaswa kuonyeshwa na malaika wa wakati wa mwisho wa kanisa. Ni wangapi wanaojua hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Hiyo ni kweli, inayopaswa kuletwa. Siri zote za Kitabu hicho cha siri zitafunuliwa kwa mjumbe wa Laodikia wa wakati huo.

Kuona kuna ubishi mwingi juu ya Mtu huyu na somo hili, nafikiri inatupasa kuliingilia, kuona kwamba Huyu ni nani. Sasa, kuna makundi mengi ya mawazo juu Yake.

Fundisho moja ni—hudai Yeye ni hadithi tu ya kubuniwa; hakuwa mtu halisi. Kwa kweli hakuwa mtu."

Na hao wengine wanasema, ya kwamba, "Ulikuwa ni ukuhani. Huo ulikuwa ukuhani wa Melkizedeki." Hilo ndilo linalowezezana sana, linaloshikilia vizuri upande huo kuliko wanavyoshikilia ule mwingine, ni kwa sababu wanasema ulikuwa ni ukuhani.

Haiwezi kuwa hivyo, kwa kuwa katika kifungu cha 4 inasema Yeye alikuwa ni Mtu, "Mtu." Kwa hiyo, kusudi awe Mtu, hana budi kuwa ni utu, "Mtu." Si utaratibu; bali ni Mtu! Kwa hiyo Yeye hakuwa tu utaratibu wa ukuhani, wala hakuwa hadithi ya uongo. Yeye alikuwa ni Mtu.

18 Na Mtu huyo ni wa Milele. Kama ukiangalia, "Hakuwa na baba. Hakuwa na mama. Hakuwa na mwanzo wa siku Zake. Na hakuwa na mwisho wa siku Zake." Na ye yote ambaye alikuwa yungali hai usiku wa leo, kwa sababu Biblia ilisema hapa, ya kwamba, "Hakuwa na baba, wala mama, mwanzo wa siku zake, wala mwisho wa uhai wake." Kwa hiyo hainabudi kuwa ni Mtu wa Milele. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Mtu wa Milele! Kwa hiyo ingeweza tu kuwa Mtu mmoja, huyo ni Mungu, maana Yeye Ndiye pekee aliye wa Milele. Mungu!

Sasa, katika I Timotheo 6:15 na 16, kama mnetaka kusoma hayo wakati mwingine, ningetaka msome hayo.

Sasa, jambo ninaloshindania ni, ya kwamba, Yeye alikuwa ni Mungu, kwa sababu Yeye ndiye Mtu pekee anayeweza kuwa asiyepatikana na mauti. Na sasa, Mungu akijibadilisha Mwenyewe katika Nafsi; Hivyo ndivyo alivyokuwa, "Hakuna baba, hana mama, hana mwanzo wa uhai wake, hakuna mwisho wa siku zake."

19 Sasa tunaona katika Maandiko ya kwamba watu wengi wanafundisha ya kwamba, "nafsi tatu katika Uungu." Kwa hiyo, huwezi kuwa na utu bila kuwa mtu. Inahitaji mtu kufanya utu.

Mhudumu Mbaptisti, majuma machache yaliyopita, alikuja, na akaja nyumbani kwangu, na kusema, "Ningetaka kukunyoosha juu ya Uungu wakati mwingine unapopata wakati." Alinipigia simu, samahani.

Nikasema, "Nina wakati sasa hivi, maana ninataka kuwa mnyofu, nasi tunaweka kando kila kitu kingine, kufanya jambo hilo."

Ndipo akaja, akasema, "Ndugu Branham, unafundisha ya kwamba kuna Mungu mmoja tu."

Nikasema, "Naam, bwana."

Akasema, "Vema," akasema, "Ninaamini kuna Mungu mmoja, bali Mungu mmoja katika Nafsi tatu."

Nikasema, "Mabwana, rudia hilo tena."

Yeye alisema, "Mungu mmoja, katika Nafsi tatu."

Nikasema, "Ulisoma wapi?" Mnaona? Naye akaniambia ch—chuo cha Biblia. Nikasema, "Ningeweza kuamini jambo hilo. Huwezi kuwa mtu bila ya kuwa utu. Na kama wewe ni utu, wewe ni nafsi moja kwako. Wewe ni mtu tofauti, binafsi."

Naye akasema, "Vema, wanatheolojia hata hawawezi kuelezea jambo hilo."

Nikasema, "Ni kwa ufunuo."

Naye akasema, "Siwezi kukubali ufunuo."

Nikasema, "Basi hamna njia kwa Mungu kuweza kukufikia kamwe, kwa sababu yamefichwa wenye hekima na akili, na kufunuliwa watoto wachanga—kufunuliwa, ufunuo kufunuliwa watoto wachanga walio tayari kuyapokea kujifunza." Nami nikasema, "Hapangekuwepo njia kwa Mungu kukufikia, umejifungia mbali Naye.

Biblia nzima ni ufunuo wa Mungu. Kanisa lote limejengwa juu ya ufunuo wa Mungu. Hakuna njia nyingine ya kumjua Mungu, ila tu kwa ufunuo. "Ambaye Mwana atamfunulia." Ufunuo; kila kitu ni ufunuo. Kwa hiyo, kukubali- ... Si kukubali ufunuo, basi wewe ni mwanatheolojia baridi tu, wala hakuna tumaini kwako.

20 Sasa, sasa, tunaona ya kwamba Mtu huyu "hakuwa na baba, hana mama, hana mwanzo wa siku zake wala mwisho wa uhai wake." Ilikuwa ni Mungu, *en morphe*.

Basi, ulimwengu—lile neno limetoka—kwa neno la Kiyunani maana yake "kubadilika," lilitumika. Akijibadilisha, *en morphe*, kutoka Mtu mmoja hadi ... Mtu mmoja; neno la Kiyunani hapo, *en morphe*, linamaanisha ... Ilichukuliwa kutoka kwenye michezo ya kuigiza, ya kwamba mtu mmoja anabadilisha kinyago chake, kumfanya mtu mwingine.

Kama vile katika—shuleni, hivi majuzi tu, ninaamini, Rebeka, kabla tu hajamaliza, walikuwa na mchezo mmoja wa kuigiza wa Shakespeare. Na kijana mmoja ilimbidi abadilishe nguo zake mara kadhaa, kwa sababu alicheza sehemu mbili ama tatu mbalimbali; lakini, mtu yule yule. Akajitokeza, mara mmoja, yeye alikuwa jeuri; na wakati alipotoka mara nyingine, alikuwa ni mtu mwingine. Na sasa neno la Kiyunani, *en morphe*, linamaanisha kwamba yeye "alibadilisha kinyago chake."

21 Na hivyo ndivyo Mungu alivyofanya. Ni Mungu yeye yule wakati wote. Mungu katika umbo la Baba, yule—yule Roho, Nguzo ya Moto. Mungu yeye yule alifanyika mwili na akakaa kwetu, *en morphe*, akatolewa apate kuonekana. Na sasa Mungu yeye yule ni Roho Mtakatifu. Baba, Mwana, Mtakatifu ... si Miungu watatu; ofisi tatu, matendo matatu ya Mungu mmoja.

Biblia ilisema, "Kuna Mungu mmoja," si watatu. Lakini hivyo ndivyo ambavyo wasingeweza ... Huwezi kulinyoosha hili na kuwa na Miungu watatu. Usingeweza kumuuzia Myahudi hilo. Nitawaambia jambo hilo. Mtu anayejua vizuri zaidi, anajua kuna Mungu mmoja tu.

22 Angalia, kama sanamu, yeye hujificha, akiwa na—na kinyago juu yake. Hivyo ndivyo Mungu alivyofanya kwa wakati huu. Imefichwa. Mambo haya yote yamefichwa, na yanapaswa kufunuliwa katika wakati huu. Sasa, Biblia inasema watafunuliwa katika nyakati za baadaye. Ni kama huyo fundi akifu—akifunika kazi yake hata wakati atakapoondoa kile kinyago kwake na ikaonekana wazi.

Na hivyo ndivyo Biblia imekuwa. Imekuwa ni kazi ya Mungu iliyofunikwa. Nalo limefichwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, na siri Yake mara saba. Na Mungu aliahidi katika siku hii, katika wakati wa kanisa hili la Laodikia, Yeye angeondoa kifuniko hicho kote na tungeweza kuliona. Ni jambo la utukufu iliyoje!

Mungu, *en morphe*, amefunikwa katika Nguzo ya Moto. Mungu, *en morphe*, katika Mtu anayelitwa Yesu. Mungu, *en morphe*, katika Kanisa Lake. Mungu juu yetu, Mungu pamoja nasi, Mungu ndani yetu; kujidhili kwa Mungu.

Kule Juu, mtakatifu, hakuna mtu angaliweza kumgusa, Yeye alikaa mlimani; na hata kama mnyama aliugusa mlima, ilimbidi afe.

Na ndipo Mungu akashuka na kubadilisha hema Yake, kisha akashuka akaishi pamoja nasi, akawa mmoja wetu. "Nasi tukamshikilia," Biblia ilisema. I Timotheo 3:16, "Bila shaka siri ya utauwa ni kuu; kwa maana Mungu alidhihirishwa katika mwili, akashikwa kwa mikono." Mungu alikula nyama. Mungu alikunywa maji. Mungu alilala. Mungu alilia. Alikuwa mmoja wetu. Mzuri, amefananishwa katika Biblia!

Huyo alikuwa ni Mungu juu yetu; Mungu pamoja nasi; sasa ni Mungu ndani yetu, Roho Mtakatifu. Si Nafsi ya tatu; Mtu yule yule!

23 Mungu alishuka na kufanyika mwili, na alikufa mauti, katika Kristo; kusudi apate kulisafisha Kanisa,

apate kuingia ndani yake, kwa ajili ya ushirika. Mungu anapenda ushirika. Hicho ndicho alichomfanyia yule mtu mara ya kwanza, ilikuwa ni kwa ajili ya ushirika; Mungu huishi peke yake, pamoja na Makerubi.

Na angalia sasa, Yeye alimfanya mwanadamu, naye mwanadamu alianguka. Kwa hiyo Yeye alishuka na kumkomboa mwanadamu, kwa sababu Mungu anapenda kuabudiwa. Neno lenyewe mungu linamaanisha "kitu cha kuabudiwa."

Na hii ambayo huja kwetu kama Nguzo ya Moto, ambayo wakati mwingine hugeza mioyo yetu, huyo ni Mungu yule yule aliyesema, "Iwe nuru," na ikawa nuru. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

24 Sasa, hapo mwanzo Mungu aliishi peke yake, pamoja na sifa Zake, kama nilivyonena habari zake asubuhi ya leo. Hayo ni mawazo Yake. Hakukuwa na kitu, ni Mungu peke yake, bali Yeye alikuwa na mawazo.

Kama tu vile mbunifu mashuhuri anavyoweza kuketi, mawazoni mwake, na kuchora kile anachofikiria ndicho atakachojenga. Kuumba, sasa, yeye hawezi kuumba. Anaweza kuchukua kitu ambacho kimeumbwa na kukifanya katika umbo tofauti; Maana Mungu ndiye njia pekee ... Mmoja tu anaweza kuumba. Bali anawaza niani Mwake atakayotenda, na hayo ni mawazo Yake, hayo ni matakwa Yake. Sasa ni wazo, halafu analinena, na ni neno basi. Na ninii—neno ni ...

Wazo, linapotamkwa, ni neno. Wazo linapotamkwa ni neno, bali haina budi kuwa wazo kwanza. Kwa hiyo, ni sifa za Mungu; ndipo linakuwa wazo, halafu neno.

25 Angalia. Wale walio na uzima wa milele usiku wa leo, walikuwa pamoja Naye na ndani Yake, katika mawazo Yake, kabla hapajakuwepo malaika, nyota, kerubi, ama cho chote kile. Huo ni Umilele. Na kama una Uzima wa Milele, daima ulikuwa nao. Si kuwoko kwako hapa, bali umbo na mfano ambao Mungu asiye kikomo...

Na kama Yeye si asiye na kikomo, Yeye si Mungu. Mungu hana budi kuwa asiye kikomo. Sisi tuna kikomo; Yeye hana kikomo. Naye alikuwa kila mahali, anajua yote, na ana nguvu zote. Kama sivyo, basi hawezi kuwa Mungu. Anajua mambo yote, mahali pote, kwa sababu ya kuenea Kwake kila mahali. Kujua yote kunamfanya Yeye awe kila mahali. Yeye ni Kiumbe; Yeye si kama upepo. Yeye ni Kiumbe; Yeye huishi katika nyumba. Lakini kwa kuwa anajua yote, akijua mambo yote, inamfanya Yeye awe kila mahali, kwa sababu Yeye anajua kila kitu kinachoendelea.

Hakuwezi kuwa na kiroboto kinachopepesa macho yake ila kile Yeye alichojua. Na alijua kabla ulimwengu haujakuwepo, ni mara ngapi kingefunga macho yake na kina shahamu kiasi gani ndani yake, kabla hapajakuwepo ulimwengu. Hilo halina kikomo. Hatuwezi kulielewa moyoni mwetu, bali huyo ni Mungu. Mungu, asiye na kikomo!

26 Na kumbuka, wewe, macho yako, umbo lako, cho chote ulichokuwa, ulikuwa katika mawazo Yake hapo mwanzo. Na jambo pekee ulilo nalo ni msemu, neno. Baada ya Yeye kuwazia jambo hilo, Yeye alilinena, nawe uko hapa. Kama sivyo, kama haukuwepo katika mawazo Yake, hamna uwezekano kamwe kwako kuwoko kule, kwa maana Yeye ndiye anayetoa uzima wa milele.

Mnakumbuka jinsi tulivyosoma Maandiko? "Si yeye atakaye, wala yeye apigaye mbio, bali ni Mungu!" Na kusudi lake la kuchaguliwa tangu zamani lipate kudumu kweli, Yeye angeweza kuchagua, kabla ya wakati wo wote, ni nani. Mungu ni mwenye mamlaka katika kuchagua Kwake. Je! Ulijua jambo hilo? Mungu ni mkuu.

Ni nani aliyekuwa huko nyuma kumwambia njia bora ya kuufanya ulimwengu? Ni nani angethubutu kumwambia Yeye alikuwa akiendesha biashara Yake vibaya?

Hata lile lenyewe—Neno lenyewe, Lenyewe, Lina mamlaka sana. Hata ufunuo una mamlaka. "Yeye humfunulia anayetaka kumfunulia." Ufunuo wenyewe, wenyewe, ni wenye mamlaka katika Mungu. Hivyo ndivyo watu wanaponda—ponda, na kurukia vitu, na kupiga vitu, na bila kujua watendavyo. Mungu ni mkuu katika kazi Zake.

27 Sasa tunamwona hapo mwanzo, sifa Zake. Na, sasa, ulikuwa pamoja Naye wakati huo. Hapo ndipo Kitabu cha Uzima huonekana.

Sasa tunasoma hapa katika Ufunuo sura ya 13, kifungu cha 8, ya kwamba yule mnyama atakayekuja juu ya nchi katika hizi siku za mwisho atawakosha watu wote wakao juu ya nchi ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha mwana Kondoo tangu kuwekwa misingi ya dunia.

Wazia jambo hilo! Kabla Yesu hajazaliwa, miaka elfu nne kabla ya Yeye kuja duniani, na miaka elfu kadhaa kabla ya wewe kuja duniani; Yesu, katika nia ya Mungu, alikufa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu, na Kitabu cha Uzima kikafanywa, na jina lako likawekwa kwenye kile Kitabu cha Uzima kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Hiyo ni Kweli ya Biblia. Mnaona, jina lako liliamriwa na Mungu na kuwekwa kwenye Kitabu cha Uzima kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.

Ulikuwa kule katika sifa Zake. Hukumbuki jambo hilo, la, kwa sababu wewe ni sehemu tu ya Maisha Yake. Wewe ni sehemu ya Mungu unapokuwa mwana ama binti ya Mungu.

Kama tu vile ulivyo sehemu ya baba yako wa duniani! Hiyo ni kweli. Wewe ni. Mwanamume hubeba hemoglobini, damu. Nayo inapoingia—kwenye lile yai, ndipo unakuwa sehemu ya baba yako, na mama yako ni sehemu ya baba yako pia; kwa hivyo ninyi nyote ni sehemu ya baba yako.

Utukufu! Hilo huondoa dhehebu nje kabisa. A-ha. Hakika hufanya hivyo! Mungu, katika yote, mahali pekee!

28 Angalia sasa sifa Zake. Ndipo zile sifa kwanza zilikuwa Mungu, wazo, sifa zenyewe, zote katika mmoja, bila kutamkwa. Ndipo alipozitamka, jambo la pili, Yeye akawa lile Neno. "Ndipo Neno akafanyika mwili akakaa kwetu."

Yohana Mtakatifu sura ya 1 na kifungu cha kwanza, angalia, hii ni, "Hapo mwanzo." Lakini, kabla, wa Milele! Angalia, "Hapo mwanzo kulikuwako Neno." Wakati ulipoanza, lilikuwa Neno. Lakini kabla halijawa Neno, lilikuwa sifa, wazo. Ndipo likatamkwa, "Hapo mwanzo kulikuwako," ule msemu, "Neno."

Sasa tunafikia mahali Melkizedeki alipo. Huyu ndiye Mtu huyu wa ajabu. "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu." "Ndipo Neno akafanyika mwili akakaa kwetu." Shikilia hilo hapo sasa, angalia.

U—Utu Wake wa kwanza ulikuwa ni Roho, Mungu, wa kimbinguni, vema, yule Milele mkuu. Pili, Yeye akaanza kufanyika mwili wa kiungu—theophania, uitwao, "Neno, mwili." Hii basi ndiyo hali aliyokuwamo alipokutana na Ibrahimu, aliitwa Melkizedeki. Yeye alikuwa katika umbo la theophania. Sasa tutalifikia hilo na kulithibitisha katika dakika chache, Bwana akipenda. Yeye alikuwa Neno.

29 Mwili wa kiungu ni kitu ambacho usingeweza kuona. Kingeweza kuwa papa hapa sasa, hata hivyo huwezi kukiona.

Ni kama tu, vema, kama televisheni. Hiyo ni katika kiwango kingine. Televisheni; watu wanatembea moja kwa moja kwenye chumba hiki sasa, wakiimba; kuna rangi, pia. Lakini jicho linatii tu zile hisi tano ... Utu wako wote uko chini ya hisi tano tu, hasa. Nawe uko chini ya yale macho yamepata kuona tu. Lakini kuna kiwango kingine kinachoweza kuonekana kwa mabadiliko, kwa televisheni.

Sasa, televisheni haitengenezi picha. Televisheni huiongoza tu kwenye mzunguko, halafu kile kioo cha televisheni kinaichukua. Lakini ile picha ipo, kwanza. Televisheni ilikuwa hapa wakati Adamu alipokuwa hapa. Televisheni ilikuwa hapa wakati Eliya alipoketi juu ya Mlima Karmeli. Televisheni ilikuwa hapa wakati Yesu wa Nazareti alipotembea katika mwambao wa Galilaya. Bali mmeanza tu kuigundua sasa. Hawangeamini zamani zile. Ungekuwa mwenda wazimu kusema kitu kama hicho. Lakini sasa imekuwa kweli.

Na ndivyo ilivyo, ya kwamba Kristo yupo hapa, Malaika wa Mungu wako hapa. Na siku moja, katika ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu unaokuja, utakuwa halisi zaidi kuliko televisheni ama cho chote kile, kwa sababu wako hapa.

Yeye hujifunua Mwenyewe katika umbo Lake kuu la yale anayodai anapoji-*En Morphe* Mwenyewe katika watumishi Wake na kujithibitisha Mwenyewe.

Sasa, huyu hapa katika umbo la Roho. Na halafu Yeye anakuja katika mfano wa ... wa *en morphe*. Sasa, Yeye alimtokea Ibrahimu, *en morphe*. Wakati Ibrahimu alipokuwa akirudi kutoka kuwaua wafalme, huyu hapa Melkizedeki akaja, akazungumza Naye.

30 Hivi majuzi katika gazeti la Tucson nilikuwa nikisoma nakala ambapo kulikuwako mwa—mwanamke aliyeendesha motokaa barabarani, yapata naamini mwendo wa maili arobaini, au hamsini kwa saa, naye akamgonga mzee mwenye kabuti. Alipiga makelele na kusimamisha gari lake. Ilimtupa hewani. Moja kwa moja huko nje kwenye jangwa tupu! Naye akakimbia kurudi kumtafuta, naye hakuwapo. Kwa hiyo yeye alifanya nini? Watu wengine nyuma yake waliona jambo hilo likitukia, walimwona mzee huyo akiruka hewani, na koti lake likipeperuka. Ndipo wakakimbia kule nyuma kumtafuta. Hawakuweza kumpata mtu huyo mahali po pote. Waliita jeshi la polisi. Polisi walikuja kuchunguza mahali hapo; hapakuwa na mtu pale.

Vema, kila mmoja wao alishuhudia ya kwamba ile motokaa ilitikisika, ikamgonga yule mtu. Akarushwa hewani, na kila mtu aliona hayo. Mashahidi, na walijaa motokaa mbili tatu, waliona ikitendeka. Nikaja kujua, miaka mitano iliyopita, kulikuwako na mzee mmoja aliyevaa koti, aliyegongwa na kuuawa mahali pale pale.

Unapoondoka hapa, hujafa. Huna budi kurudi, hata kama wewe ni mwenye dhambi, na kuhukumiwa kulingana na matendo yaliyofanywa katika mwili. "Kama maskani hii ya duniani ikiharibiwa, tuna moja inayongoja." *En morphe*, hilo ndilo neno.

31 Sasa, Mungu, katika hatua hii ya ... Ni hatua hii ya uumbaji Wake, baadaye aliyeumbwa katika mwili, Yesu. Kutoka kwa nini? Tangu ule mwanzo mkuu, Roho, ndipo akashuka akawa Neno, akijitokeza Mwenyewe. Neno bado halijifanyi Lenyewe, limenenwa tu, *en morphe*, baadaye anakuwa mwili, Yesu, anayekufa, kuonja mauti kwa ajili yetu sisi sote wenye dhambi.

Wakati Ibrahimu alipokutana Naye, Yeye alikuwa Melkizedeki. Yeye anafunua hapa yale sifa zote zitafanya katika mwisho wake, kila mwana wa Ibrahimu. Kila mwana wa Imani atafanya jambo lile lile kabisa. Bali nataka kuangalia jinsi itupasavyo kuja.

Pia, tunamwona akifunuliwa hapa katika Ruthu na—na Boazi, kama Mkombozi aliye Jamaa wa Karibu, namna ilivyombidi kuja kuwa mwili.

32 Sasa tunaona sifa, wana wa Roho Wake, bado hawajaingia katika mwili wa umbo la Neno. Lakini, mwili wa kiungu (theophania); Huu mwili uko chini ya mamlaka ya Neno na arabuni, ukingojea arabuni, kubadilishwa kwa mwili.

Sasa, tofauti kati Yake na wewe, kama mwana. Mnaona, Yeye alikuwa, hapo mwanzo, Neno, mwili *en morphe*. Yeye aliingia na kuishi katika huo, katika Utu wa Melkizedeki. Ndipo, baadaye, hatukusikia tena juu ya Melkizedeki, kwa sababu Yeye alifanyika Yesu Kristo. Melkizedeki alikuwa Kuhani, bali Yeye alifanyika Yesu Kristo. Sasa, wewe uliliepa hilo. Kwa sababu, katika hali hiyo, Yeye alijua mambo yote, nawe hujaweza kujua hilo bado.

Ulikuwa kama Adamu, kama mimi, ulifanyika kutoka kwenye sifa ukafanyika mwili, upate kujaribiwa. Lakini wakati uhai huu utakapokwisha hapa, "Kama maskani hii ya duniani ikiharibiwa, tuna moja tayari inayongoja." Huko ndiko tunakoenda; hilo ni Neno. Ndipo tunaweza kuangalia nyuma na kuona yale tuliyojanya. Sasa hatuelewi hayo. Hatujawahi kamwe kuwa Neno; tumekuwa tu watu wa mwili, si Neno.

Na tazama kwa makini, inakuonyesha wazi ya kwamba hautakuwa Neno kamwe isipokuwa ulikuwa wazo hapo mwanzo. Hilo linathibitisha kuchaguliwa tangu asili kwa Mungu. Mnaona? Huwezi kuwa Neno isipokuwa wewe ni wazo. Ilibidi uwe katika mawazo, kwanza.

Lakini, mnaona, kusudi upate kuvumilia majaribu, ilikubidi kuupita ule mwili wa kiungu. Ilikubidi kuja hapa katika mwili, kujaribiwa na dhambi. Halafu basi, kama ukisimama, "Wote alionipa Baba watakuja Kwangu, nami nitamfufua katika siku za mwisho." Mnaona, ilibidi uwe wa kwanza.

33 Halafu basi, mnaona, Yeye alishuka moja kwa moja, mstari wa kawaida, kutoka sifa hadi ... Kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, jina lake limeandikwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo. Ndipo, kutoka hapo, Yeye akawa Neno, ule mwili wa kiungu, ambao ungeweza kuonekana, ukatoweka. Na halafu Yeye akawa mwili na akarudi tena, akaufufua mwili ule ule katika hali ya utukufu.

Lakini wewe uliupita ule mwili wa kiungu na ukawa mwanadamu wa mwili, upate kujaribiwa na dhambi. Halafu basi, "Kama maskani hii ya duniani ikiharibiwa, tuna moja tayari inayongoja." Bado hatuna miili.

Lakini, tazama! Wakati mwili huu unapompokea Roho wa Mungu, Uzima usiopatikana na mauti ndani yako, unatiisha mwili huu chini ya Mungu. Haleluya! "Yeye aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi; hawezi kutenda dhambi." Warumi 8:1, "Basi sasa, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu; hawaenendi kwa kufuata mambo ya mwili, bali kwa Roho." Ndivyo hivyo. Mnaona, hiyo huutiisha mwili wako.

Haikubidi kusema, "Loo, laiti ningaliacha tu kunywa pombe! Kama ningeweza tu ..." Ingia tu katika Kristo, na yote yamekwisha, mnaona, mnaona, kwa sababu mwili wako unamtii Roho. Hauko tena chini ya mambo ya dunia; yamekufa. Yamekufa; dhambi zako zimezikwa katika ubatizo; nawe u kiumbe kipya katika Kristo. Na mwili wako, ukimtii Roho, jaribu kuishi maisha mazuri.

34 Kama vile ninyi wanawake mnavyodai mna Roho Mtakatifu, na mkitoka nje hapa na kuvaa kaptura na kadhalika, mngewezaje kufanya hivyo? Roho wa Mungu aliye ndani yako angewezaje kukufanya utende jambo kama hilo? Haiwezekani kabisa kuwa hivyo. Hakika, haiwezekani. Yeye si roho mchafu; Yeye ni Roho Mtakatifu.

Na halafu mnapotiishwa chini ya Roho huyo, inatiisha utu wako wote chini ya Roho huyo. Na huyo Roho si kingine ulimwenguni ila hili Neno Mbegu Iililodhihiriswa, au lilolohuishwa haleluya, lililofanywa hai. Na Biblia iliposema, "Usitende *hili*," mwili huo unaligeukia upesi; hamna swali. Hakuna swali.

Na ni kitu gani? Ni amana ya ufufuo. Mwili huu utafufuliwa tena, kwa sababu tayari umeanza. Wakati mmoja ulikuwa chini ya dhambi, na matope na uharibifu, lakini sasa una arabuni; umegeuka wa Kimbinguni. Sasa, hiyo ndiyo arabuni ya kwamba utanyakuliwa. Ni arabuni.

Mtu mgojwa anapolala akifa, hamna kilichobakia isipokuwa kifo, hayo tu ndiyo yanayoweza kutendeka. Nimeona vivuli vya watu walioliwa na kansa pamoja na kifua kikuu, na kuwaona watu hao baadaye wakiwa wazima na wenye nguvu. Kama hakuna uponyaji wa Kiungu, basi hakuna ufufuo, maana

uponyaji wa Kiungu ni arabuni ya ufufuo. Amina!

Mnajua pesa za arabuni ni nini, sivyo? Ni malipo ya awali. "Alijeruhiwa kwa makosa yetu; kwa kupigwa Kwake sisi tumepona." Angalia jinsi lilivyo la ajabu! Tunampenda.

35 Sasa, mwili huu umetiishwa chini ya Roho. Bado hatujaingia katika umbo la Neno, bali tungali katika hali ya mwili, bali tunatii Neno. Mauti katika mwili itatupeleka kule.

Jambo lile lile tu, wazia juu ya mtoto mchanga. Unaweza kumchukua mwanamke, haidhuru yeye ni mwovu namna gani, wakati akiwa mjamzito na anakaribia kuwa mama. Angalia, kabla mtoto huyo hajazaliwa, sijali namna mwanamke huyo alivyo katili, anakuwa mwema sana. Kuna kitu fulani kuhusu sauti yake ... Mna kitu kwake kinachoonekana kitauwa sana, kuona maskini mama akikaribia kuwa mama kwa kupata mtoto. Kwa nini? Mwili huo mdogo, sasa, haujakuwa hai bado. mnaona, kitu ulicho tu, ni nyama na misuli. Huko kuruka kidogo, hiyo ni misuli tu inayumba. Lakini unapotoka tumboni, Mungu huupulizia pumzi ya uhai, na ndipo anapaza sauti. Mnaona, kama tu—hakika kama kunao mwili wa kawaida, unaotengenezwa, kunao mwili wa kiroho tayari kuupokea mara unapofika hapo.

36 Halafu, wakati mtu anapozaliwa mara ya pili, kutoka Mbinguni, anakuwa mtoto mchanga wa kiroho katika Kristo.

Na, halafu, wakati joho hili la mwili linapodondoshwa, kuna mwili wa kawaida, mwili wa kiungu, mwili usiotengenezwa kwa mikono, wala kuzaliwa na mwanamke, ambao tunauendea.

Ndipo mwili huo unarudi na kuuchukua mwili uliotukuzwa.

Hiyo ndiyo sababu Yesu alienda kuzimuni alipokufa na kuwahubiri nafsi zilizokaa kifungoni; akarudia ule mwili wa kiungu. Loo, ajabu sana! Mungu ashukuriwe!

Korintho wa pili 5:5 "Mwili wetu ulio wa dunia hii ukiharibiwa, maskani haya ya dunia hii, tunalo jengo lingine." Mnaona, tumeruka hilo tukaja moja kwa moja kutoka kwa Mungu, zile sifa, kufanyika mwili tukashawishiwe na kujaribiwa kwa dhambi kama Adamu alivyofanywa. Lakini wakati kujaribiwa kwa Neno Lake kumekwisha, basi tunapelekwa kwenye mwili huu ambao ulitayarishwa kwa ajili yetu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Ni Neno pale ambapo tuliliruka, kuja moja kwa moja, hapa chini kushashiwa na kujaribiwa. Kama tungepitia hayo, kusingekuwako na majaribu; tungejua mambo yote. Hiyo ndiyo sababu Yesu alijua mambo yote, maana Yeye alikuwa Neno kabla Yeye hajawa mwili. Ndipo tunakuwa Neno.

Hapa tunaumbwa kwa sura ya Neno tupate kuwa washiriki wa Neno, tuwe washiriki wa Neno, tule Neno, kwa kuchaguliwa kimbele tangu mwanzo; mnaona, hiyo cheche ndogo ya uhai ilikuwa ndani yako tangu mwanzo ulipoanza safari yako. Wengi wenu mnaweza kuikumbuka. Mlijiunga na kanisa *hili* na kujiunga na kanisa *lile* na kujaribu *hili* na *lile*; hamkutosheka. Hiyo ni kweli. Lakini siku moja ulilitambua tu. Sawa.

37 Usiku uliopita nilikuwa nikifundisha mahali fulani, nafikiri ilikuwa huko California au Arizona, karibu ... Naamini nimehadithia hadithi hiyo ndogo hapa kuhusu mtu aliyemwatamisha kuku yai la tai. Na yule tai alipoanguliwa, alikuwa ndege wa kuchekesha sana ambaye vifaranga hao walipata kumwona. Lakini, alitembea kila mahali. Yeye alikuwa—alikuwa mwenye sura baya zaidi miongoni mwao, kwa maana hangalielewa kamwe namna huyo kuku angalia na kukwaruza kwenye zile taka na kula. Asingeweza kupata wazo hilo. Angesema, "Njoo huku na ule, mpenzi!" Lakini, yeye alikuwa ni tai; hakula hivyo kamwe. Hakikuwa chakula chake.

Kwa hiyo angeweza kuwashika nzige na kadhalika, mwajua, na kuwaita hao kuku wadogo. Na hao kuku wote wadogo wangeenda pamoja, wakipiga kelele, na kula. Lakini maskini yule tai mdogo asingeweza kufanya hivyo. Haiku—haikuonekana sawa kwake.

Kwa hiyo siku moja mama yake akaja kumtafuta.

38 Naye angemsikia huyo kuku akilia. Angejaribu awezavyo, lakini asingeweza kufanya hivyo. Alijaribu kulia kama vifaranga wa kuku, lakini hangeweza kufanya hivyo. Mnaona, yeye alikuwa ni tai. Yeye, kwanza, alikuwa ni tai. Alikuwa tu ameanguliwa chini ya kuku.

Hiyo ni kama washiriki wa kanisa. Kila ... Hivyo ndivyo ilivyo; huwa ni mmoja miongoni mwa kundi zima, aliye kweli.

Lakini siku moja mamaye akaruka, naye akapaza sauti. Yeye alitambua jambo hilo. Hilo lilisikika sawa. Kwa nini? Yeye alikuwa ni tai, kwanza.

Hivyo ndivyo ilivyo na Injili, ama Neno, ama Nguvu za Yesu Kristo. Wakati mtu amechaguliwa tangu awali kwa ajili ya Uzima wa Milele, husikia huo mlilo wa kweli, mlilo wa Mungu, hakuna kitu kinachoweza kumzuia.

Kanisa linaweza kusema, "Siku za miujiza zimekwishakupita," kidoko, kidoko, kidoko. "Simama hapa na ule *hiki*, na simama hapa na ule *kile*."

Huo uchafu wa ghala hautamfaa tena. Ameondoka! "Mambo yote yanawezekana!" Yeye anaondoka ardhini.

Hiyo ndiyo sababu, shida ya Wakristo wengi sana siku hizi, hawawezi kuondoa miguu yao kutoka ardhini.

Yule mama mzee akasema, "Mwanangu, ruka! Wewe ni tai. Njoni huku juu niliko."

Akasema, "Mama, kamwe sikuwahi kuruka, maishani mwangu."

Akasema, "Vema, ruka! Wewe ni tai, kwanza. Wewe si kuku." Kwa hivyo akaruka kwa mara yake ya kwanza na kupigapiga mabawa yake; hakufaulu sana, bali aliondoka ardhini.

Hivyo ndivyo tunavyofanya. Tunamkubali Mungu kwa imani, kwa Neno lililoandikwa. Kuna kitu fulani mle ndani; ni huo Uzima wa Milele. Ulichaguliwa tangu asili.

Babu yake na bibi yake walikuwa tai. Yeye alikuwa ni tai, huko nyuma kabisa. Tai haichanganyiki na mambo mengine. Yeye si chotara; hapana. Yeye ni tai.

39 Ndipo, baada ya wewe kutambua kwamba Neno la Mungu hasa lilikuwa Chakula cha Tai, ndipo ukaacha jambo lingine. Wewe basi umeumbwa kuwa mfano ulio hai wa Mungu aliye hai. Ulisikia kutoka kwenye mwili wako wa kiungu. "Kama mwili huu wa duniani ukiharibiwa, tuna mmoja unaongoja."

Unasema, "Hiyo ni kweli, Ndugu Branham?"

Vema, hebu na tuchukue tai wachache na tuwaangalie kwa dakika chache. Kulikuwa na jina, mtu aliyeitwa Musa. Kila mtu anajua ya kwamba nabii anaitwa tai, katika Biblia.

Kulikuwa na nabii jina lake Musa. Na siku moja Mungu alimwita, wala asingemruhusu aingie nchini, naye—naye akafia kwenye Mwamba. Malaika walimchukua wakamzika.

Kulikuwako na mtu mwingine, tai, hata haikumlazimu kufa. Yeye alienda tu kuvuka Yordani, na Mungu akatuma gari likashuka; na vazi hili la mwili aliliangusha, na kufufuka na kupata tuzo ya milele.

Miaka mia nane baadaye, miaka mia nane baadaye, kwenye Mlima wa Kugeuzwa, hapa walisimama hao watu wawili. Mwili wa Musa ulikuwa umeoza kwa mamia ya miaka, lakini hapa alikuwa katika umbo hata hadi Petro, Yakobo, na Yohana walimtambua. Amina! "Kama maskani hii ya duniani ikiharibiwa," kama wewe ni sifa ya Mungu iliyodhihirishwa hapa duniani, "una mwili unaongojea baada ya kuuacha ulimwengu huu." Hao hapo, wamesimama juu ya Mlima wa Kugeuzwa, katika mwili wao. Kwa kuwa, walikuwa manabii ambao Neno liliwajia.

40 Pia hebu na tumwangelie nabii mwingine, wakati mmoja, jina lake Samweli. Yeye alikuwa mtu mashuhuri. Alikuwa amewafundisha Israeli; Aliwaambia hawapaswi kuwa na mfalme. Yeye alisema, "Je! Nimewahi kuwaambia jambo moja katika Jina la Bwana ila lile lilitimia?"

Wakasema, "La. Kila kitu ambacho daima umesema katika Jina la Bwana kilitimia."

Yeye alikuwa nabii, naye akafa.

Yapata miaka mitatu ama minne baadaye, mfalme alipata shida; hiyo ilikuwa kabla ya Damu ya Yesu Kristo kumwagwa. Yeye alikuwa paradiso. Na mchawi wa Endoni akampandishia mtu, kumfariji Sauli. Na yule mchawi alipomwona amesimama, akasema, "Naona Mungu akitoka katika nchi."

41 Huku mtu huyu amekufa, kazikwa, na kuozea kaburini, huku amesimama pale kwenye pango lile amevikwa joho lake la kinabii, naye alikuwa bado yu nabii, amina, kwa kuwa alisema, "Mbona umeniita usingizini mwangu, nawe umekuwa adui wa Mungu?" Mwangalie akitabiri. "Kesho usiku, kufikia wakati huu, utakuwa pamoja nami." Yeye alikuwa angali ni nabii, ingawa alikuwa ameondoka kwenye mwili huu.

Mnaona, akaja hapa na alikuwa sehemu ya Neno hilo, naye akatoka kwenye uhai wa mwili huu akaingia katika mwili aliotengenezewa kabla kuwekwa misingi ya ulimwengu. Yeye aliingia katika mwili wa kiungu, ambao ulikuwa ni Neno. Mnalipata? Humo ndimo waumini wote huenda tunapotoka humu.

Halafu, katika hali hiyo, pazia linaondolewa. Mnaona, wewe ni Neno, pia, unapoingia mle. Kama mtoto mchanga; kama nilivyosema muda mfupi uliopita ...

Sasa angalia. Mungu asifiwe kwa ajili ya kufunguliwa kwa Mihuri hii, ndilo ombi langu, kujua mambo haya!

42 Sasa ufunuo wa kweli wa Melkizedeki unaonekana. Nini? Yeye alikuwa Mungu, Neno, kabla

hajafanyika mwili; Mungu, Neno. Maana, ilibidi awe; hakuna mwingine angeweza kuwa asiyepatikana na mauti kama Yeye. Mnaona, nilikuwa na baba na mama; ulikuwa nao, pia. Yesu alikuwa na baba na mama. "Lakini Mtu huyu hakuwa na baba, wala hakuwa na mama." Yesu alikuwa na mwanzo wa siku Zake; Mtu huyu hakuwa nao. Yesu alitoa uhai Wake; Mtu huyu asingeweza, kwa sababu Yeye alikuwa Uzima. Na ni Mtu yule yule wakati wote. Natumaini Mungu atakufunulia. Mtu yule yule, wakati wote.

Angalia cheo Chake, "Mfalme wa haki." Sasa, Waebrania 7:2, "Mfalme wa haki, na Mfalme wa amani." Yeye ni wafalme wawili. Sasa angalia, Waebrania 7:2, "Mfalme wa haki, na Mfalme wa amani." Yeye ni wafalme wawili kule. Sasa, kwa kuwa alikuja katika mwili na mwili wake wa utukufu ukatwaliwa kule juu, katika Ufunuo 21:16 Yeye anaitwa Mfalme wa Wafalme. Yeye ni wote watatu, pamoja. Mnaona, Mfalme Mungu, Mfalme Theofania, Mfalme Yesu. "Yeye ni Mfalme wa wafalme."

Yote yanatimizwa, kama tu nafsi, mwili, na roho, yote huja kufanya kitu kimoja.

Pia, Yeye ni Baba, ambaye alikuwa wa kwanza; Mwana; na Roho Mtakatifu, Roho.

"Mfalme wa haki," sifa za Roho; theofania, "Mfalme wa—wa amani," theofania; na katika mwili Yeye alikuwa "Mfalme wa wafalme," Mtu yule yule.

43 Wakati ule mwili wa kiungu, Musa alipomwona, Kutoka 33:2, Yeye alikuwa mwili wa kiungu. Musa alitaka kumwona Mungu. Alikuwa amesikia sauti Yake, alimsikia akinena naye, akamwona kwenye kijiti pale, kama Nguzo kubwa ya Moto. Naye akasema, "Wewe ni nani? Ninataka kujua Wewe ni Nani." Musa alisema. "Nitaweka ..." "Kama utaniruhusu nikuone Wewe, ningetaka kuuona uso Wako."

Yeye alisema, "Hakuna mtu awezaye kuuona uso Wangu." Yeye alisema, "Nitaweka mkono Wangu juu ya macho yako, nami nitapita. Nawe unaweza kuona mgongo Wangu, bali si uso Wangu." Mnaona? Na wakati alipofanya hivyo, ulikuwa ni mgongo wa Mwanadamu; ulikuwa ni mwili wa kiungu. Ndipo lile Neno lililomjia Musa, "MIMI NIKO," hilo lilikuwa ni Neno. Neno lilimjia Musa katika mfano wa Nguzo ya Moto katika kijiti kilichowaka moto, "MIMI NIKO."

Kama vile Neno kutoka kwenye theolojia ... kutoka theofania, hasa. Samahani. Yeye alimjia Ibrahimu kama Mwanadamu, chini ya mwaloni. Sasa angalia pale. Kukaja mtu kwa Ibrahimu, watatu, na wakaketi chini ya mwaloni, hao watatu. Pia angalia, baada ya Yeye kuzungumza na Ibrahimu ...

44 Kwa nini alikuja? Ibrahimu, maana alikuwa ndiye mwenye ile ahadi pamoja na ujembe wa kujiliwa na mwana, na pia alikuwa nabii wa Neno la Mungu aliyekuwa akiamini Neno la Mungu, akiyataja yale yaliyokuwa kinyume kama kwamba si kinyume Mnaona jinsi Neno lilivyo kamilifu? Neno lilimjia nabii. Mnaona, kulikuwako na Mungu katika mwili wa kiungu. Na Biblia ilisema, "Neno humjia nabii." Na hapa kulikuwa na—na Neno katika mwili wa Kiungu.

Sasa unasema, "Huyu alikuwa ni Mungu?"

Ibrahimu alisema ilikuwa hivyo. Yeye alisema jina Lake, lilikuwa, alimwita Elohimu. Sasa katika Mwanzo 1, mnaona, "Hapo mwanzo *Elohimu* aliumba mbingu na nchi." Katika Mwanzo 18, tunaona ya kwamba—ya kwamba Ibrahimu alimwita Mtu huyu ... aliyeketi pale na kuzungumza naye, na angeweza kumwambia siri za moyo wake, kumwambia kile Sara alichokuwa akiwazia nyuma Yake. Ibrahimu akasema, "Ni Elohimu." Yeye alikuwa katika umbo la theofani. Mnalipata? Angalia baada ya ...

45 Sasa tunaona ya kwamba Yeye wakati huo alikuwa katika umbo la theofania. Yeye alimwita, "Bwana Mungu, Elohimu." Sasa, katika Mwanzo 18, tunaona ya kwamba hiyo ni kweli.

Sasa angalia Ibrahimu. Kulikuwa na watatu pamoja, lakini Ibrahimu alipokutana na hao watatu, alisema, "Bwana wangu."

Lakini wakati Lutu, huko chini Sodoma; wawili wao walishuka wakaenda kule, na Lutu akaona wawili wao wakija, naye akasema, "Mabwana wangu." Mnaona, kulikuwa na nini? Kwanza, Lutu hakuwa nabii, hiyo ni kweli, wala hakuwa mjumbe wa wakati huo, kwa hiyo hakuwa na ufunuo wowote wa Huyu. Ni kweli kabisa. Lutu angeweza kuwaita "mabwana." Dazani yao, bado angaliweza kusema, "mabwana."

Lakini haidhuru Ibrahimu aliona wangapi, ilikuwa bado ni Bwana mmoja. Huyu hapo Mungu. Huyu alikuwa ni Melkizedeki.

Angalia, baada ya vita kwisha, Melkizedeki alitumikia ushirika wa mtoto Wake; wazia hilo, sehemu Yake Mwenyewe! Sasa tunataka kuona hapa. Katika mfano hapa, ushirika, unaonekana hapa. Baada ya vita, Yeye alijitoa Mwenyewe, kwa sababu ushirika ni sehemu ya Kristo. Na baada ya mapambano kwisha, baada ya kupigwa vikali sana, ndipo unashiriki Kristo, unakuwa sehemu ya Kiumbe hiki. Mnalipata?

46 Yakobo alipigana mieleka usiku kucha, wala asingemwachilia mpaka Yeye ambariki. Hiyo ni kweli. Kupigania Maisha! Na baada ya vita kwisha, basi Mungu anakupa sehemu Yake Mwenyewe. Huo ndio

ushirika Wake wa kweli. Mkate mdogo na mkate mwembamba huwakilisha Hilo tu. Hupaswi kulichukua isipokuwa umeshindana vilivyo na kuwa sehemu ya Mungu.

Kumbukeni, wakati huu ushirika haukuwa umeanzishwa, si hadi kabla ya kifo cha Yesu Kristo, mamia na mamia na mamia ya miaka baadaye.

Lakini Melkizedeki, baada ya mtoto Wake Ibrahimu kushinda, Melkizedeki alikutana naye na kumpa divai na mkate; ikionyesha ya kwamba baada ya vita hivi vya duniani kwisha, tutakutana Naye mbinguni na kula ushirika tena. Itakuwa ni Karamu ya Arusi. "Sitakunywa divai tena ama kula ya matunda, hata nitakapokula na kunywa pamoja nanyi upya katika Ufalme wa Baba Yangu." Hiyo ni kweli?

47 Angalia tena, Melkizedeki alienda kukutana na Ibrahimu kabla hajarudi nyumbani. Ni mfano mzuri jinsi gani hapa tulio nao! Melkizedeki akikutana na Ibrahimu kabla hajarudi nyumbani, baada ya vita.

Tunakutana na Yesu hewani, kabla hatujafika Nyumbani. Hiyo ni kweli. Wathesalonike wa Pili wanatuambia ya kwamba, kwa kuwa, "tunakutana Naye hewani." Mfano mzuri wa Rebeka akikutana na Isaka, kondeni, wakati wa jua kupunga. "Tunakutana Naye hewani." Wathesalonike wa Pili wanatuambia hivyo. "Kwa maana sisi tulio hai, tuliosalia, hatutawatangulia wala kuwazuia hao waliokwisha kufa; kwa kuwa parapanda ya Mungu italia; waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza; sisi tulio hai na tuliosalia tutanyakuliwa pamoja nao, kumlaki Bwana hewani." Ni kamilifu, mifano hii yote.

Kwa hiyo, ule mwili wa kiungu, kama umekufa na kuingia katika huo mwili wa kiungu, (ni jambo gani linalotukia?) Mwili wa kiungu unakuja duniani kuchukua mwili uliokombolewa. Na iwapo umo humu hewani, unachukua mwili kuulaki ule mwili wa kiungu, ndivyo hivyo, na kunyakuliwa kwenda kumlaki Bwana hewani.

Ni nani huyu Melkizedeki ila Mungu!

48 Sasa tunaona hapa dhahiri siri kamili ya maisha yetu katika safari, na mauti, na mahali tunapoenda baada ya kufa. Pia, kuchaguliwa tangu zamani kunaonekana wazi hapa. Sasa sikilizeni tunapofundisha jambo hili, kwa makini.

Hatua za—za kusudi la Milele alilokuwa nalo katika siri Yake sasa zimefunuliwa. Angalia, bado kuna hatua tatu za ukamilifu. Kama tu vile anavyokomboa ulimwengu; kwa njia ile ile anayolikomboa Kanisa Lake. Yeye huwakomboa watu katika hatua tatu. Sasa angalia. Kwanza ni kuhesabiwa haki, kama Luther alivyohubiri; pili, utakaso, kama Wesley alivyohubiri; tatu, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli. Ndipo unakuja Unyakuo!

Sasa, ulimwengu, Yeye aliukomboaje ulimwengu? Alichofanya kwanza ulipotenda dhambi, aliusafisha kwa ubatizo wa maji. Hiyo ni kweli. Kisha akamwaga damu Yake juu Yake kutoka msalabani na kuutakasa na kuuita Wake Mwenyewe. Halafu basi Yeye anafanya nini? Kama vile alivyoarua ulimwengu wote kotoka kwako na kufanya upya vitu vyote kwa ubatizo wa moto wa Roho Mtakatifu, Yeye pia ataufanya upya ulimwengu. Nao utachomwa moto na kuondolea mbali kila viini kwa umbali wa maili milioni kadhaa kwenda juu, na kila kitu kitafagiliwa mbali. Na halafu kuna Mbingu Mpya na Nchi Mpya, kama tu vile wewe ni kiumbe kipya katika Kristo Yesu wakati Roho Mtakatifu anapokushika. Mnaona, haya basi, jambo hilo lote ni dhahiri tu liwezavyo kuwa. Kila kitu kiko katika tatu.

49 Kuzaliwa kwa kawaida ni katika tatu. Ni kitu gani cha kwanza kinachotokea kwa mwanamke kupata mtoto? Ni kitu gani hutoka kwanza? Maji. Ni nini kinachotokea baadaye? Damu. Utaratibu unaofuata ni upi? Uhai. Maji, damu, roho.

Ni kitu gani kinachotendeka kwa mmea huo? Unaoza. Jambo la kwanza ni nini? Ubuu. Ni nini kinachofuata? Kishada. Ni nini kinachofuata? Kapi. Ndipo punje inatokea hapo. Ni hatua zake tatu tu, mpaka inafika kwenye punje. Hiyo ni kweli kabisa.

Mungu huthibitisha hilo. Hilo daima limekuwa ni kweli. Mungu huthibitisha kwamba ni kweli. Inaonyesha wazi wazi ya kwamba aliyechaguliwa kimbele ndiye tu anayefikiriwa katika ukombozi. Mlilipata? Hebu niseme jambo hilo tena. Waliochaguliwa tangu asili ndio pekee wanaofikiriwa katika ukombozi. Huenda watu wakawa wanajifanya, wanafikiri wamekombolewa, bali ukombozi halisi ni wale waliochaguliwa tangu asili. Kwa sababu, neno lenyewe kukomboa linamaanisha "kurudisha." Hiyo ni kweli? *Ukombozi* ni kitu ... *Kukomboa* chochote, ni, "kukirudisha mahali pake pa asili." Haleluya! Kwa hiyo ni wale tu waliochaguliwa tangu asili ndio watakaorudishwa, kwa sababu hao wengine hawakutoka Kule. Mnaona, "kurudisha!"

50 Tukiwa wa Milele pamoja Naye, hapo mwanzo ... Ule Uzima wa Milele uliokuwa nao, wazo Lake la ulivyokuwa, tu, Yeye alitaka wewe ... Alitaka nisimame mimbarani, tuseme. Alikutaka uketi kitini usiku wa leo. Ndipo tunatumikia kusudi Lake la Milele. Na yule aliyeeondoka nyumbani, alikuja tu duniani kulitumikia kusudi Lake. Hiyo ni kweli? Vema. Halafu, baada ya kumalizika, inarudishwa katika hali ya utukufu; umekomaa na kurudishwa tena.

Si ajabu Paulo angesema walipokuwa wakijenga gogo la kukatia kichwa chake. Alisema, "U wapi, Ewe mauti, uchungu wako? Ewe kaburi, ushindi wako uko wapi? Lakini Mungu ashukuriwe atupaye ushindi!" Akasema, "Mauti, niambie mahali ambapo unapoweza kunifanya nipige mayowe! Kaburi, niambie jinsi utakavyonishikilia! Kwa kuwa, Mimi ni mmiliki wa Uzima wa Milele." Amina! Yeye alitambua jambo hilo. Mauti, kuzimu, kaburi, hakuna kitu kingeweza kumshikilia. Na hakuna kitu kinachoweza kutudhuru, tuna Uzima wa Milele! Alitambua alikuwa amebarikiwa kwa Uzima wa Milele.

51 Ni kama tu tone la umande. Kama nikielewa, ni ... Sijui mengi sana kuhusu kemia. Bali halina budi kuwa ni ku—kuganda kwa unyevu ama hewa. Na usiku unapokuwa baridi na wenye giza, hilo huanguka kutoka mbinguni na kuanguka ardhini. Limeanguka kutoka mahali fulani. Bali asubuhi inayofuata kabla jua halijachomoza, limekaa pale, maskini tone hilo, likitetemeka. Lakini hebu jua lichomoze, tazama likimetameta. Ni furaha. Kwa nini? Jua litaliita moja kwa moja kurudi lilikutoka.

Na hivyo ndivyo ilivyo kwa Mkristo. Halleluya! Tunajua tunapoingia katika Uwepo wa Mungu, kitu fulani ndani yetu kinatumbia ya kwamba tunatoka mahali fulani, nasi tunarudi tena kwa Nguvu hizo zinazotuvuta.

Tone hilo la umande humetameta na kuangaza na kupaza sauti, kwa sababu linajua limetoka kule juu na lile jua litaliina juu kule tena.

Na mtu ambaye ni sifa ya Mungu, aliyezaliwa na Mungu anajua halleluya, anapompata Mwana wa Mungu, atainuliwa atoke hapa siku moja. "Kwa maana nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta watu wote Kwangu." Amina!

52 Sasa tazama! Sasa tunaona Melkizedeki na kwa nini Mariamu hakuwa mama Yake. Hiyo ndiyo sababu Yeye alimwita "mwanamke," si mama. "Yeye hakuwa na baba," kwa kuwa Yeye alikuwa Baba, Baba wa milele, wale watatu katika Mmoja. "Hakuwa na mama," hakika hakuwa. Hakuwa na baba, kwa kuwa Yeye alikuwa ni Baba. Kama vile yule mshairi alivyosema wakati mmoja, akimpa sifa kubwa Yesu, alisema:

MIMI NIKO aliyenena na Musa katika kijiti kilichowaka moto,
MIMI NIKO Mungu wa Ibrahimu, Nyota ya Asubuhi Inayong'aa.
MIMI NIKO Alfa, Omega, mwanzo tangu mwisho.
Mimi ni uumbaji wote, na Yesu ndilo hilo Jina. (Hiyo ni kweli.)
Loo, mnasema mimi ni nani, Wao husema nilitoka wapi,
Je, mnajua Baba Yangu, Au je, mnaweza kusema Jina lake? (Halleluya!)

Hilo ndilo Jina la Baba! Naam, "Nimekuja katika Jina la Baba Yangu, wala hamkunipokea." Mnaona? Hakika, ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

53 Na huyu Melkizedeki akawa mwili. Yeye alijifunua Mwenyewe kama Mwana wa Adamu alipokuja, kama Nabii. Yeye alikuja katika majina matatu ya Mwana; Mwana wa Adamu, Mwana wa Mungu, Mwana wa Daudi.

Wakati alipokuwa hapa duniani, Yeye alikuwa Mwanadamu, kutimiza Maandiko. Musa alisema, "Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii kama mimi." Kwa hiyo ilimbidi kuja kama Nabii. Yeye hakusema, kamwe hakusema, "Mimi ni Mwana wa Mungu." Yeye alisema, "Mimi ni Mwana wa Adamu. Unamwamini Mwana wa Adamu?" Maana, hivyo ndivyo ilivyombidi kushuhudia, kwa sababu hivyo ndivyo alivyokuwa.

Sasa Yeye amekuja katika Jina la mwana mwingine, Mwana wa Mungu; asiyeonekana, ni Roho.

Na wakati atakapokuja tena, Yeye ni Mwana wa Daudi, kuketi juu ya kiti Chake cha enzi.

54 Sasa wakati alipokuwa hapa na akafanyika mwili, aliitwa, "Mwana wa Adamu." Sasa, Yeye alijitambulishaje ulimwenguni kama Mwana wa Adamu, yule Nabii?

Siku moja nilikuwa nikisimulia hadithi ya Petro na Andrea, ndugu yake. Walikuwa ni wavuvi, na baba yao Yona alikuwa mzee mashuhuri mwaminio. Siku moja walisema aliketi kando ya mtumbwi. Yeye alisema, "Wana, mnajua jinsi ambavyo tumeomba wakati tulipohitaji samaki." Walikuwa wavuvi wa kibiashara. Yeye alisema, "Tumemtumaini Mungu, Yehova, kwa ajili ya maisha yetu. Nami ninazeeka sasa; Siwezi kukaa nanyi wavulana kwa muda mrefu zaidi. Nami daima, kama waamini wote wa kweli, nimeutazamia wakati ambapo Masihi huyo atakuja. Tumekuwa na kila namna ya uongo, lakini anakuja Yule halisi, siku moja." Naye akasema, "Masihi huyu atakapokuja, sitaki ninyi wavulana kudanganywa. Masihi huyu hatakuwa mwanatheolojia tu. Yeye atakuwa ni Nabii, kama nabii wetu Musa, ambaye tunamfuata, alisema."

Sasa, Myahudi yeyote atamwamini nabii wake. Yeye anafundishwa kujua jambo hilo. Na kama nabii akisema cho chote ambacho ni kweli, basi hiyo ni kweli. Lakini Mungu alisema, "Kama kuna mmoja miongoni mwenu, wa kiroho, ama nabii, Mimi Bwana nitajitambulisha Kwake. Na asemayo yakitimia, ndipo msikizeni na kumwogopa, bali kama hayatimii, basi msimwogope kamwe." Mnaona? Kwa hiyo hilo lilikuwa ni —ni thibitisho la nabii.

55 "Kwa hiyo Musa alikuwa kweli ni nabii aliyethibitishwa, naye akasema, 'Bwana Mungu wenu atawainulia, miongoni mwenu, kutoka kwa ndugu zenu, Nabii kama mimi. Na wote wasiomsikia watakatiliwa mbali na watu.'" Yeye alisema, "Sasa, watoto, kumbukeni, ya kwamba, kama Waebrania, tunaamini manabii wa Mungu waliothibitishwa."

Sasa sikilizeni kwa makini. Usilikose. Naye akasema, "Masihi ajapo, mtamjua, kwa maana Yeye atakuwa Nabii-Masihi. Sasa, walisema imekuwa ni miaka mia nne. Hatukuwa na nabii tangu Malaki, bali atakuwa!"

Siku moja, baada ya kifo chake, miaka michache, mwanawe Andrea alikuwa akitembea kwa miguu ufukoni. Naye akasikia mtu wa porini kutoka jangwani akisema, "Huyo Masihi amesimama miongoni mwenu sasa." Yule tai mkubwa aliyeinuka nyikani na kuruka kule, kasema, "Masihi yuko miongoni mwenu sasa hivi. Hatujamjua bado, bali Yeye anasimama miongoni mwenu. Nitamjua, kwa sababu nitaona ishara inayotoka Mbinguni."

Siku moja alisema, "Huyo hapo, tazama, yuko Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu!"

Akaenda zake ... mtu huyu akaenda, akamtafuta ndugu yake. Yeye alisema, "Simoni, ninataka uje hapa; tayari tumempata Masihi."

"Loo, endelea, Andrea! Unajua vizuri zaidi ya hilo!"

"Loo, ninajua. Lakini, kwamba, Mtu huyu ni tofauti."

"Yuko wapi? Yeye alitoka wapi?"

"Yesu wa Nazareti."

"Huo mji mdogo, mwovu? Mbona, Yeye asingeweza kutoka mahali pabaya, pachafu namna hiyo."

"Njoo tu uone."

Hatimaye nikamshawishi ashuke aje siku moja. Kwa hiyo wakati alipokuja mbele ya huyu Masihi, Yesu amesimama pale, akizungumza na watu. Wakati alipoenda mbele Zake, Yeye alisema, "Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona." Hilo lilitosha. Alipata funguo za Ufalme. Kwa nini? Yeye alijua ya kwamba Mtu huyo hakumjua. Na Yeye alimjuaje, na yule baba mzee mcha Mungu aliyemfundisha jinsi ya kumwamini Masihi?

56 Kulikuwa na mtu aliyesimama pale, jina lake Filipo. Loo, alisisimka sana! Yeye alimjua mtu mwingine, aliyekuwa akisoma Biblia pamoja naye. Akaenda zake, akazunguka kilima, naye akamkuta huko nje kwenye shamba lake la mizeituni. Alikuwa akipiga magoti, akiomba. Walikuwa wamepata masomo mengi ya Biblia pamoja, kwa hiyo akaja pale. Naye akasema, baada ya kumaliza kuomba, alisema, "Njoo, uone ni Nani tuliyemwona; Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu. Yeye ni Masihi tunayemtazamia."

Sasa, naweza kumsikia Nathanieli akisema, "Nini, Filipo, nakusudia hujatumbukia kilindini, sivyo?"

"Loo, la. La. Sasa hebu niwaambie. Mwajua, tumekuwa tukisoma Biblia pamoja, na nabii alisema Masihi angekuwa nini?"

"Angekuwa ni Nabii."

Je, unakumbuka yule mzee mvuvi uliyenunua samaki kwake, ambaye hakuwa na elimu angaa ya kuandika jina lake, aliyetwa Simoni?"

"Naam. A-ha."

"Akaja. Nanyi mnajua nini? Huyu Yesu wa Nazareti alimwambia ya kwamba jina lake lilikuwa Simoni, alibadilisha jina lake likawa Petro, ambalo ni 'jiwe dogo' na kumwambia baba yake alikuwa nani."

"Vema," akasema—akasema, "Sijui. Kuna kitu chema kinachoweza kuja toka Nazareti?"

Yeye alisema, "Hebu tusizungumze juu ya jambo hilo; njoo tu uone." Hilo ni wazo zuri, "Njoo uone."

Kwa hiyo huyu hapa Filipo anakuja, akimleta Nathanaeli. Na wakati alipoenda kule, Yesu labda amesimama, akizungumza, labda akiwaombea wagonjwa kwenye mstari wa maombi. Na wakati alipofika mahali Yesu alipokuwa, Yesu alimwambia, na kusema, "Tazama Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake."

57 Sasa, unasema, "Vema, ilikuwa ni namna alivyokuwa amevaa." Loo, la. Watu wote wa mashariki huvalia vivyo hivyo. Angeweza kuwa ni Msiria, ama angekuwa kitu kingine chochote; ndevu, vazi.

Yeye alisema, "Tazama Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake," kwa maneno mengine, "mtu mwaminifu, mkweli."

Vema, hilo lilimtoa pumzi Nathanieli. Naye akasema, "Rabi," ambalo maana yake ni, "mwalimu." "Rabi, ulinjua lini? Ulijuaje mimi ni Myahudi? Ulijuaje kwamba nilikuwa mwaminifu, sina hila?"

Akasema, "Kabla Filipino hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona." A-ha! Maili kumi na tano mbali, upande ule mwingine wa nchi, siku iliyotangulia.

Yeye alisema nini? "Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe u Mfalme wa Israeli!"

58 Bali kulikuwako wale makuhani, wenye kiburi, wagumu, kasema, "Mtu huyu ni Belzebuli, mpiga ramli."

Yesu alisema, "Nitawasamehe kwa jambo hilo."

Sasa, kumbukeni, hawakusema hilo kwa sauti kuu, bali walilisema mioyoni mwao. "Naye akatambua mawazo yao." Hiyo ni kweli. Hivyo ndivyo Biblia inavyosema. Liite kushirikiana mawazo ukitaka, bali Yeye —Yeye alijua mawazo yao.

Naye akasema, "Nawasamehe kwa jambo hilo. Lakini siku moja Roho Mtakatifu atakuja na kutenda jambo lile lile," baada ya kuondoka Kwake; "kunena neno moja dhidi Yake, haitasamehewa kamwe katika ulimwengu huu au ulimwengu ujao." Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Sasa, hao walikuwa ni Wayahudi.

Ndipo siku moja alikuwa na haja ya kwenda Samaria. Lakini kabla tu hatujafanya jambo hilo, tulimpata yule mwanamke, ama ninii ...

59 Mtu huyo, alipopitia kwenye lango lililoitwa Mzuri, ya kwamba aliponywa. Naye Yesu alijua hali yake, na akamwambia, "Chukua kitanda chako uende nyumbani." Naye akafanya hivyo, na akapona.

Ndipo tunaona, Wayahudi, baadhi yao walimpokea. Wengine waliamini jambo hilo; wengine hawakuamini. Kwa nini hawakuamini jambo hilo? Hawakuwa wamekusudiwa Uzima. Hawakuwa sehemu ya sifa hiyo.

Sasa kumbukeni, hao walikuwa makuhani na watu mashuhuri. Naye Yesu ... Wazia juu ya hao wanatheolojia na makuhani, watu ambao usingeweza kupata kasoro maishani mwao. Yesu alisema, "Ninyi ni wa baba yenu Ibilisi, na kazi zake mnazifanya." Kasema, "Kama ungekuwa wa Mungu, ungeniamini Mimi. Kama hamwezi kuniamini Mimi, amininii—aminini kazi nizifanyazo Mimi; zinashuhudia Mimi ni nani."

Sasa, Biblia ilisema, ya kwamba, "Yesu ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Yesu alisema, "Kazi nizifanyazo Mimi, yeye aniaminiye Mimi, naye atazifanya." Hiyo ni kweli? Angalia, huyo alikuwa Melkizedeki halisi sasa.

60 Sasa angalia, tena, kulikuwako na jamii tatu tu za watu.

Mmenisikia nikisema nilikuwa mbaguzi. Mimi ndiye. Wakristo wote ni mbaguzi; si ubaguzi wa rangi, bali ubaguzi wa roho. Rangi ya mtu ya ngozi yake haina uhusiano wowote naye. Yeye ni mwana wa Mungu kwa Kuzaliwa. Lakini Mkristo, Mungu alisema, "Nitengeni!" "Tokeni kati yao," na kadhalika. Yeye ni mbaguzi, wa uchafu, kati ya mema na mabaya.

Bali tazama, walikuwa na ubaguzi wakati huo, ubaguzi wa rangi, ambao ni Wasamalia.

Na kuna jamii tatu tu za watu duniani; kama tunaamini Biblia; hao ni watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi. Hao ndio wana watatu wa Nuhu. Sisi sote tulitoka hapo. Hiyo ni kweli. Hiyo inaturudisha sote kwa Adamu, ambayo inatufanya sote ndugu. Biblia ilisema, "Kwa damu moja Mungu aliumba mataifa yote." Sisi sote ni ndugu, kupitia kwenye kijito cha damu. Mtu mweusi anaweza kumpa mtu mweupe damu, ama vinginevyo. Mtu mweupe anaweza kumpa yule—yule Mjapani, mtu wa manjano, ama Mhindi, mtu mwekundu, ama chochote kile, ama Myafeti, ama chochote kile, angeweza kumpa damu, maana sisi sote ni damu ile ile. Rangi ya ngozi yetu, mahali tulipoishi, haikuwa na uhusiano wowote nayo.

Lakini wakati tunapotengwa, ni wakati tunapotoka ulimwenguni, kama vile Yeye alivyowatoa Israeli kutoka Misri. Hapo ndipo tunapotengwa na mambo ya ulimwengu.

61 Sasa, walikuwa ni watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi. Na kama tunaweza kufuatilia vizazi kule nyuma, tungeona Wa-Anglo-Saxon, kule walikotoka. Sasa, huyo alikuwa ni Myahudi ... Msamaria, ambaye alikuwa nusu Myahudi na Mmataifa, aliyeolewa na Mataifa katika matendo ya Baalam, na Moabu. Walikuwa ni Wasamaria. Na kulikuwako na Wayahudi na Mataifa.

Sasa, sisi Anglo-Saxon hatukuwa na uhusiano wo wote na jambo hilo. Hatukuamini Masihi yeyote, wala chochote kingine. Hatukuwa tukimtarajia mmoja. Tuliingizwa baadaye.

Yesu alikuja kwa walio Wake, na walio Wake hawakumpokea. Naye akawaambia wanafunzi Wake, "Msiende katika njia ya Mataifa, bali nendeni kwa kondoo wa Israeli waliopotea." Na Yeye alienda tu kwa kondoo waliopotea wa Israeli. Na angalia, Yeye alijidhihirisha Mwenyewe kama Mwana wa Adamu, mbele ya Wayahudi. Wakamkataa.

Sasa, Msamaria, akiwa nusu Myahudi na Mmataifa, waliamini pia, na walikuwa wakimtazamia Masihi.

Hatukumtazamia. Tulikuwa makafiri, tukiwa na marungu mgongoni mwetu, tukiabudu sanamu; wa Mataifa.

62 Lakini sasa siku moja, Yohana Mtakatifu 4, Yeye alihitaji kupitia Samaria, akienda zake kwenda Yeriko. Lakini alikuwa amezunguka Samaria. Na wakati alipokuwa akienda kule juu, aliketi kwenye kisima nje ya mji uitwao Sikari. Na kisima kile, iwapo umewahi kuwa pale, ni mahali padogo panapovutia kama hapa hivi. Na kuna chemchemi ya umma pale, ya maji, ambapo wote wanakuja. Nao wanawake wanakuja asubuhi, wanachukua vyungu vyao vya maji, na kuviweka juu ya vichwa vyao, na kimoja kwenye kila nyonga, na kutembea nacho sawa kabisa wawezavyo, kamwe hawatamwaga hata tone; wakiongea mmoja kwa mwingine. Kwa hiyo, wangepanya hivyo, watu wangepuka huko nje.

Kwa hiyo hii ilikuwa yapata saa tano mchana. Kwa hiyo akawatuma wanafunzi Wake mjini, kununua mlo, chakula. Na walipokuwa wameondoka ...

63 Kulikuwako na mwanamke aliyekuwa na sifa mbaya. Tungemwita, leo, mwanamke rangi nyekundu, ama malaya. Alikuwa na waume wengi mno. Kwa hiyo wakati Yesu alipokuwa ameketi pale, mwanamke huyu alitoka yapata saa kumi na moja. Mnaona, asingeweza kuja pamoja na wanawali walipokuja asubuhi kuchukua maji yao ya kuoshea; ilimbidi kungojea mpaka wote ... Hawakuchanganyikana kama wanavyofanya sasa. Alikuwa ametiwa alama. Kwa hiyo basi, akaja kuteka maji, kwa hiyo akachukua tu ile winchi ya kale, na kuweka kulabu kwenye ule mtungi, na akaanza kuushusha.

Alimsikia Mtu fulani akisema, "Mwanamke, nipe maji ninywe." Sasa, kumbukeni, huyu ni Melkizedeki. Huyu ni Yesu, jana, Mwana wa Adamu.

Naye akaangalia kote, naye akamwona Myahudi. Kwa hiyo akasema, "Bwana, si vema kwa Myahudi kumwomba Msamaria cho chote. Mimi ni mwanamke Msamaria, kwa hiyo umekosea. Hukupaswa kuniuliza kitu kama hicho. Hatuna uhusiano mmoja kwa mwingine."

Yeye alisema, "Lakini kama ungalijua ni Nani aliyekuwa akisema nawe, ungeniomba Mimi maji."

Akasema, "Utayatekaje? Kisima ni kirefu, wala huna kitu cha kutekea."

Yeye alisema, "Maji ninayotoa ni Maji ya Uzima, yakibubujika Uzima wa Milele."

Alizungumza naye mpaka akapata jinsi hali yake ilivyokuwa. Na basi ni ... Angalia alivyomwambia sasa, "Nenda kamwite mumeo uje hapa."

Naye akasema, "Sina mume."

Yeye alisema, "Umesema kweli, kwa kuwa umekuwa na watano, na huyo unayeishi naye sasa si wako. Kwa hiyo, katika jambo hili, umesema kweli."

Angalia tofauti kati ya mwanamke huyo na kundi hilo la makuhani. Alijua zaidi juu ya Mungu kuliko kundi hilo lote la makuhani walivyokuwa wameungana.

64 Akasema, "Bwana, naona ya kwamba Wewe ni Nabii." Akasema, "Hatujapata mmoja kwa miaka mia nne. Sasa, tunajua ya kwamba Masihi yuaja. Na wakati Masihi atakapokuja, hilo ndilo atakalofanya." Hiyo ilikuwa ni ishara ya Masihi, kwa kuwa Yeye alikuwa ni Mwana wa Adamu. Kasema, "Hivyo ndivyo atakavyofanya atakapokuja. Huna budi kuwa nabii Wake."

Yeye alisema, "Mimi Ndiye." Hakuna mtu mwingine angeweza kusema jambo hilo.

Yeye alianguka mtungi huo wa maji na kukimbilia mjini, na kusema, "Njoo, umwone Mtu aliyeniambia yale niliyofanya. Je! Huyu si ndiye Masihi hasa?"

Sasa kumbukeni, Yeye aliahidi kufanya jambo lile lile mwishoni mwa jamii ya Mataifa.

Wayahudi walikuwa na miaka elfu nne kumtazamia Masihi huyo, miaka elfu nne ya kufundisha kwamba Yeye angekuja, na yale angefanya alipofika kule, nao wakashindwa kumwona, ama wakashindwa kutambua jambo hilo. Na wakati alipojitambulisha Mwenyewe katika maneno yale yale ya Biblia aliyosema angefanya, wakati alipokuwa mwili wa kiungu kisha akafanyika mwili na kukaa miongoni mwao, walishindwa kuuona, na kuziita kazi Zake kazi za Ibilisi.

65 Sasa tumekuwa na miaka elfu mbili ya mafundisho, tukishuka kupitia kanisa Katoliki la Kirumi, baada

ya mitume. Ndipo tukaja kupitia Katoliki ya Kirumi, ya Kiyunani, na kadhalika, tukafikia kwenye wakati wa Luther, na Wesley, kadhalika, madhehebu mia tisa mbalimbali yakishuka. Walikuwa na nyakati hizi zote, wakifundisha.

Sasa Yeye aliahidi, kabla tu wakati wa mwisho haujaja, ya kwamba picha ya Sodoma na Gomora ingetukia tena, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa wakati wa mwisho, Mwana wa Adamu atajifunua. Mwenyewe tena." [Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.]

"Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena; hata hivyo mtaniona, kwa maana Mimi," kiwakilishi nafsi, "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari, mwisho wa dunia. Nitakuwa pamoja nanyi." Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Mnaona?

Mnaona, *Msamaria* alikuwa, kwa kweli, kutokana na mahubiri yangu ya jana usiku, alikuwa ni Hajiri, mnaona, mfano uliopotoshwa. Myahudi alikuwa ni Sara, ama alikuwa Wasara. Lakini Mmataifa ni wa Mariamu, Uzao wa Kifalme, Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu.

66 Sasa imeahidiwa ya kwamba katika siku hizi za mwisho, ya kwamba, Mungu huyu huyu, Kristo huyu huyu, angerudi hapa na kujifunua Mwenyewe kama Mwana wa Adamu.

Kwa nini? Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Na kama angewaacha hao Wayahudi wapite, na kuwapa ile ishara ya Masihi, halafu afikie mwisho wa mafundisho ya Mataifa na kuwaacha waingie tu kwenye theolojia, Yeye angekuwa asiye haki. Hana budi kufanya jambo lile lile, kwa sababu Biblia ilisema, katika thir- ... Waebrania 13:8, "Yeye ni yeye yule."

Naye ameahidi katika Malaki 4, na Maandiko yote mbalimbali, ya kwamba, siku za mwisho, kanisa lingekuwa limeketi kama tu lilivyo leo, na ulimwengu ungekuwa.

Angalia ulimwengu siku hizi. Angalia hali ya Sodoma. Angalia matetemeko ya nchi mahali mbalimbali, na mambo yanayotendeka. Angalia kanisa na machafuko yaliyomo, ya Babeli. Mwangalie mjumbe wake, Oral Roberts na Billy Graham.

G-r-a-h-a-m, mara ya kwanza tulipopata kuwa na mjumbe, kwa makanisa yote, kwamba jina lake lingeshia katika h-a-m, kama vile Ibrahimu. A-b-r-a-h-a-m ni herufi saba. G-r-a-h-a-m ni herufi sita. Yuko wapi? Kwa ulimwengu. Sita ni namba ya mwanadamu. Mwanadamu aliumbwa siku ya sita. Lakini saba ni namba ya Mungu.

67 Sasa waangalie huko chini kule Sodoma. Na kuna hao wajumbe wao kule chini wakizungumza nao.

Lakini basi uko wapi ule Uzao wa kifalme wa Ibrahimu? Iko wapi ishara yao, aliyosema? "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma," ambapo Mungu alishuka na kudhihirishwa katika mwili wa kibinadamu, na kumwambia yale Sara aliyokuwa akiwazia huko nyuma moyoni mwake, katika hema nyuma Yake, ishara ya mwisho kabla ya ulimwengu wa Mataifa kuangamizwa kwa moto. . Nalo Kanisa lina ishara yake ya mwisho kabla ulimwengu wote haujaangamizwa, ufalme huu wa Mataifa uangamizwe kwa moto na ghadhabu ya Mungu. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

Ya kwamba Melkizedeki alikuwa mwili, alijiwakilisha Mwenyewe katika mwili wa mwanadamu; na halafu baadaye akafanyika mwili. Na sasa, usiku wa leo, ni yeye yule, jana, leo, na hata milele. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

Ni nani huyu Melkizedeki, basi, ambaye ni yeye yule jana, leo ... "Kamwe hakuwa na baba, kamwe hakuwa na mama; Yeye kamwe hakuwa na mwanzo wa siku zake, kamwe hakuwa na mwisho wa maisha." Naye alikutana na Ibrahimu, na alifanya ishara ya namna gani? Ndipo wakati alipofanyika mwili, Yeye alisema yangejirudia tena kabla tu ya wakati wa mwisho. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Ninaamini jambo hilo. ["Amina."]

Hebu na tuombe.

68 Mungu mpenzi, ninaamini Maandiko, ya kwamba Wewe umesema ulikuwa "yeye yule jana, leo, na hata milele." Na kwa uaminifu moyoni mwangu, Bwana, ninajua ya kwamba jambo fulani liko karibu kutukia. Siwezi kabisa kulitambua. Ninaogopa kusema lolote, Bwana. Wewe unajua moyo wa mtumishi Wako.

Na ni mara ngapi kote kote kwenye zile nyakati ulipotuma vitu, watu wakashindwa kuvitambua. Mwanadamu daima anamsifu Mungu kwa yale aliyofanya, na kusema ni mambo gani makuu atakayofanya, lakini akipuuza yale anayofanya. Ndivyo imekuwa kupitia nyakati zote. Kwa nini kanisa la Kirumi lilishindwa kumwona Mtakatifu Patrick kama nabii wa Mungu? Ni kwa nini walimwua Joan wa Arc wakati yeye alikuwa ni—nabii mke, wakamchoma kama mchawi? Baba, kila mara ni yaliyopita. Umeyaficha wenye hekima na akili. Si ajabu Wewe uliwaambia hao makuhani, "Mnayapamba makaburi ya manabii, na ninyi ndio mliowaweka mle ndani." Baada ya wao kuondoka, wanajiona kosa lao. Daima wanakutesa Wewe, Bwana, katika hali yo yote utakayoingia.

69 Ninaomba, usiku wa leo, Mungu, mara moja tu zaidi. Kesho tumepangiwa kuwa ... kwenda Tucson. Sehemu zingine za ulimwengu, miji mingine hatuna budi kuhubiri. Lakini, Mungu Mpendwa, huenda kukawa na wageni hapa usiku wa leo ambao kamwe hawaja ... Wamesikia Maneno yakihubiriwa, lakini kamwe hawajaliona likidhihirishwa.

Kama nilivyokuuliza hapo mwanzo. Wakati hao wanafunzi, Kleopa na rafiki yake, wakija kutoka Emau, walikuwa wakitembea njiani, na Wewe ulitoka kichakani ukaanza kuzungumza nao, baada ya ufufuo, ukawahubiria. Mbona, Yeye alisema, "Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito. Hivi hamjui ya kwamba Kristo alipaswa kupata mateso haya, kisha aingie katika utukufu Wake?" Lakini bado hawakutambua jambo hilo. Siku nzima walitembea pamoja Nawe, na bado hawakukujua. Lakini usiku mmoja ...

Usiku ukaja, wakakuzuia kuingia. Walipoingia kwenye ile nyumba ndogo ya wageni na kufunga milango, ndipo ulifanya jambo fulani jinsi tu ulivyofanya kabla ya kusulibishwa Kwako, nao wakatambua ilikuwa ni Kristo aliyefufuka. Katika dakika chache Wewe ulikuwa nyuma ya mapazia ukaondoka. Upesi wakakimbia na kuwaambia wanafunzi, "Bwana amefufuka kweli!"

Baba, Mungu, ninaamini ya kwamba Wewe ungali hai. Ninajua Wewe ndiwe. Nawe umetuhakikishia jambo hilo mara nyingi sana. Ungeweza tu kufanya jambo hilo mara nyingine tena kwa ajili yetu, Bwana? Kama tulipata neema mbele Zako, hebu na itukie mara nyingine tena. Mimi ni mtumishi Wako; hawa ni watumishi Wako hapa ndani. Bwana, yote niliyosema hayangefikia ... Neno moja tu kutoka Kwako lingekuwa zaidi ya nilivyosema katika siku hizi tano za usiku, ama jumbe tano. Ingekuwa zaidi, neno moja tu kutoka Kwako. Mbona usinene, Bwana, ili kwamba watu wapate kujua ya kwamba nimewaambia Kweli? Tujalie, Mungu. Ninaomba katika Jina la Yesu, hili mara nyingine tena. Amina.

70 Sasa, sikujui. Ninawajua watu fulani. Namjua huyu mvulana anayeketi hapa. Namjua Bill Dauch ameketi papo hapo. Ninataka kuninii ... Huyu hapa Ndugu Blair, Rodney Cox. Ni vigumu kuona huko nje.

Upande huu, moja kwa moja wakati wa sasa siwezi kumwona mtu, kwa kweli, ninayemjua.

Sasa ni wangapi humu ndani wanaojua ya kwamba mimi ni mgeni kwenu? Inueni mikono yenu, mnajua ya kwamba sijui lolote kuwahusu, inueni mikono yenu pande zote mbili.

Ni wangapi humu ndani walio na kasoro fulani, ama kitu fulani ambacho mnajua ambacho sijui kitu juu yake? Mwaweza kuinua mikono yenu.

Sasa, haingewezekana kabisa, kabisa kabisa kwangu kujua cho chote kukuhusu. La sivyo, basi, itabidi itoke kwenye ufunuo fulani wa Roho.

Na kwa kuwa nimewaambia usiku huu wote, na usiku wa leo, ya kwamba Yeye hajafa; Yeye yuko hapa, na ameahidi kufanya jambo lile lile. Na aliahidi ya kwamba kungekuja wakati katika siku za mwisho, kulingana na Malaki 4 na kulingana na Mtakatifu Luka, ambapo Yeye angeonekana tena katika umbo la kibinadamu miongoni mwa watu Wake na kufanya mambo yale yale, na kufunua jambo lile lile, ishara ile ile ya Masihi. Ni wangapi wanaojua jambo hilo, ninyi wasomaji wa Biblia, mnajua hiyo ni Kweli? Sema, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Lazima wote wawe wasomaji wa Biblia.

Sasa, ninajua ni geni kwa watu siku hizi, bali hata hivyo ni Kweli. Hiyo ndiyo sababu hawakumjua Yesu wa Nazareti. Walijua kanuni zao za kanisa, bali hawakumjua. Lakini Yeye alikuja tu jinsi Biblia ilivyosema; si mwanatheolojia, si kasisi. Yeye alikuja kama Nabii, na walio Wake hawakumpokea.

71 Sasa, kama Mungu atatimiza Neno Lake, na kama ikitokea kwamba ... itatukia juu ya mtu fulani ninayemjua, basi nita—nitampata mtu mwingine. Mnaona, ninataka mtu fulani ambaye simjui. Nami nawatakeni muombe.

Sasa, angalia, kulikuwa na maskini mwanamke mmoja wakati mmoja aliyekuwa na udhaifu. Alikuwa ametumia pesa zake kwa ajili ya madaktari; wasingeweza kumfaa kitu. Naye akasema moyoni mwake, "Kama ninaweza kugusa mavazi ya Mtu huyo, nitapona." Mnakumbuka hadithi hiyo? Na kwa hiyo wote hao walijaribu kumfanya akae nyuma, bali alijikaza mpaka akagusa vazi Lake, akarudi na kuketi chini.

Sasa sikilizeni kwa makini. Na ndipo alipofanya jambo hilo, wakati mwanamke huyo alipofanya jambo hilo, Yesu aligeuka na kusema, "Ni nani aliyenigusa?"

Mbona, Petro mtume alimkemea. Huenda alisema kitu kama, "Bwana, usiseme jambo kama hilo. Watu wataamini kuna kasoro Kwako. Kwa sababu, wakati ulipowaomba kula mwili Wako na kunywa Damu Yako, tayari wanafikiri kuna kasoro. Nawe unasema, 'Ni nani aliyenigusa?' Mbona, umati wote unakugusa."

Yeye alisema, "Naam, bali ninaona ya kwamba nguvu zimenitoka." Huo ulikuwa ni mguso wa aina nyingine. Sasa, kila mtu anajua ya kwamba nguvu ni "nguvu." "Nikawa mnyonge; nguvu zimeniacha."

Naye akaangalia kila mahali kwenye wasikilizaji mpaka akampata maskini mwanamke huyo, na kumwambia kuhusu kutokwa kwake na damu. Naye akahisi mwilini mwake ya kwamba kutokwa na damu

kulikuwa kumekoma. Hiyo ni kweli? Naye akasema, “Imani yako imekuokoa.”

Sasa, neno la Kiyunani hapo ni *sozo*, ambalo linamaanisha kabisa “kuokolewa,” kimwili ama kiroho, vivyo hivyo. Yeye “aliokoa.” Yeye ni—Yeye ni Mwokozi wako.

72 Sasa, kama huyo alikuwa ni Yeye jana, na jinsi alivyotenda, kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa miongoni mwa watu, Masihi aliyeahidiwa; na hivyo ndivyo alivyojitambulisha Mwenyewe, na kuahidi kwa Biblia, Yeye angefanya jambo lile lile sasa; si Yeye, si ingebidi kufanya jambo lile lile?

Unasema, “Je! Yeye alisema kuhusu kuonya wagonjwa?” Naam!

Waebrania, Biblia ambayo ndiyo kwanza nisome, ilisema ya kwamba, “Yesu Kristo sasa ni Kuhani wetu Mkuu anayeweza kuchukuliana nasi katika mambo yetu ya udhaifu.” Ni wangapi wanaojua hilo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.” — Mh.] Biblia ilisema hivyo. “Yeye ni Kuhani Mkuu sasa anayeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu.” Basi kama Yeye ni Kuhani Mkuu yule yule aliyekuwa wakati huo, angefanyaje sasa? Ingebidi kutenda vile vile alivyotenda wakati huo, kama Yeye ni Kuhani Mkuu yule yule. Sasa, huenda ...

Mimi si Kuhani Mkuu wenu. Huenda ukanigusa, na ingekuwa tu kama kumgusa mume wako, ama ndugu yako, ama chochote kile, mwanamume.

73 Bali wewe acha imani yako imguse, na uangalie kile kinachotukia. Sasa, kama mimi ni mtumishi wa Mungu na nimewaambia Kweli, Mungu atathibitisha hilo kuwa ni Kweli. Na hilo lingethibitisha ya kwamba Yesu Kristo anaishi usiku wa leo, amesimama hapa. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.” — Mh.]

Sasa, una imani, upande mmoja tu kwa wakati mmoja, upande mmoja. Mna imani huko nje. Afadhali nikae kwenye maikrofoni hapa, kwa sababu hawawezi kunisikia.

Mtu fulani anamwangalia tu Mungu, na kusema, “Mungu, mtu huyo hanijui. Yeye hajui lolote kunihusu mimi. Mimi ni mgeni kabisa kwake. Lakini hebu imani yangu ikuguse Wewe, Bwana. Nawe unajua shida yangu ni nini, Bwana. Unajua yote kunihusu. Unajua mimi ni nani, vile vile kama ulivyojua Petro alikuwa nani, vile vile ulivyomjua Nathanaeli, kama vile ulivyojua shida ya mwanamke huyo kwa kutokwa na damu. Na mtu huyu ananiambia ya kwamba Wewe ni 'yeye yule jana, leo, na hata milele.' Basi, Bwana, jalia imani yangu ikuguse.”

Na kama Yeye atafanya jambo hilo, na kujithibitisha Mwenyewe hapa, ni wangapi wenu mtakaomwamini kwa moyo wenu wote; kama atafanya jambo hilo angalau mtu mmoja, ama wawili, ama watatu, kwa—kwa ajili ya ushuhuda? [Kusanyiko linasema, “Amina.” — Mh.] Mungu akubariki.

74 Sasa, Baba Mungu, hii kabisa haimo mikononi mwa mtu ye yote. Ingekuwa ni jambo la kimbinguni. Kwa hiyo ninaomba ya kwamba utanisaidia sasa, Bwana. Niko mikononi Mwako. Nitendee upendavyo. Katika Jina la Yesu. Amina.

Sasa, msiwe na wasiwasi. Sema tu kwa unyenyekevu, kwa uchaji, “Bwana, nitakutumikia. Na hilo litakuwa ni kweli, ya kwamba, kama ninaweza kugusa vazi Lako, basi Wewe nena kupitia kwa mtu huyo. Hilo litanithibitishia ya kwamba aliyosema ni Kweli.” Hiyo ni kweli?

Ni wangapi waliopata kuona picha ya Nuru hiyo? Yuko kote nchini, kila mahali. Sayansi imelichukua na kulichunguza, na kila mahali. Sasa, Yeye yuko papa hapa sasa; Yeye yule aliyesema juu ya Ndoa na Talaka, Yeye yule aliyekuwa mlimani, alitikisa vilima huko nyuma, Yeye yule aliyeko hapa chini mtoni mwaka wa '33, yeye yule jana, leo, na hata milele. Yeye ni yeye yule.

75 Sasa, kuna mwanamke, naye anatambua sasa ya kwamba jambo fulani limetukia. Nuru hiyo inaning'inia moja kwa moja juu yake. Ameketi papa hapa, amevaa sweta ya kijani kibichi, ama chochote kile. Simjui mwanamke huyo. Nadhani hatufahamiani. Hiyo ni kweli. Je! Unaamini ya kwamba Mungu ... Una—unahitaji kitu fulani, na unaamini ya kwamba Mungu anaweza kunifunulia shida yako ni nini? Na kama akifanya hivyo, basi unajua itabidi iwe ni nguvu ya kimbinguni, kwa sababu mimi sikujui wewe. Na itabidi ije kwa njia ya kimbinguni.

Inategemea kile unachofikiri ndicho. Unaweza kuchukua upande wako pamoja na makuhani, uliite “ibilisi,” ama unaweza kuchukua upande wa mwaminio na kuliita “Mungu.” Chochote unachoamini, hapo ndipo thawabu yako itakapotoka.

Kama Mungu atanifunulia shida yako, je! Utamkubali kama upatanisho wako—wako kwa ajili ya shida hiyo? Sijui shida ni nini. Lakini ninajua, nanyi mnajua, ya kwamba jambo fulani linaendelea.

Sasa, sasa hebu niwaambie namna mnavyojisikia, na ndipo mtajua; hisi halisi ya joto, tamu, raha. Ninalitazama moja kwa moja. Ni ile Nuru, Nuru ya manjano inayong'inia kutoka kwa huyu mwanamke.

Naye mama huyo ana ugonjwa wa tumbo. Ni namna fulani ya vimbe, kama, tumboni mwake. Yeye

hatoki hapa. [Huyo dada anasema, "Sawa." — Mh.] La. Umetoka mbali na hapa sivyo? Hiyo ni kweli. Umetoka Wisconsin. Hiyo ni kweli? Hakika. Sasa umeponywa. Imani yako imekuponya.

Sasa niambie yule mwanamke alimgusa nani? Nina umbali wa yadi ishirini na tano kutoka kwake. Alimgusa Yesu Kristo, Kuhani Mkuu. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

76 Ninamtazama mwanamke niliyezungumza naye. Mwanamke huyu, ninamwangalia moja kwa moja, maana anamwomba kwa bidii sana kwa ajili ya mwanamume. Aliniambia alikuwa na mwanamume ... Yeye hakuniambia lo lote kuhusu jambo hilo.

Lakini jina lake ni Bibi Waldrop. Yeye anatoka Phoenix. Alifufuka katika wafu, na daktari wake akaja na eksirei na akaonyesha kansa moyoni. Alikufa kwenye mstari wa maombi. Imekuwa muda gani, Bibi Waldrop? Miaka kumi na minane iliyopita, naye ameketi pale usiku wa leo, ushuhuda ulio hai. Daktari wake amekuja mkutanoni, akaleta ... Kasema, "Mwanamke anawezaje kuishi?" Lakini huyo hapo, wala hakuna dalili yake.

Yeye amemleta mtu fulani, naye anamwomba. Sasa, anakufa, kwa ugonjwa wa kisukari. Sasa, hilo nililijua. Lakini kwa kuwa unaomba ... Unajua sijui yeye ni nani, Bibi Waldrop.

Ametoka Missouri, na jina lake ni Bw. Cooper. Hiyo ni kweli. Sasa, unaamini, unaweza kurudi nyumbani na uwe mzima, bwana. Ni juu yako, kama utaamini.

77 Huyu hapa mwanamke, naye anaugua ugonjwa wa pumu, matatizo. Yeye hatoki hapa. Ameketi huko nje kwenye umati, papo hapo. Natumaini atapata ... Yeye hatoki hapa. Ametoka Georgia. Bibi McKenny. Je! Unaamini kwa moyo wako wote, na unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Simama kwa miguu yako, kama wewe ni mgeni kwangu na hiyo ni kweli. Yesu Kristo anakuponya. Unaamini?

[Ndugu Branham ameupa mgongo wake kusanyiko — Mh.]

Kwa mgongo wangu, kuna mtu anayeketi nyuma yangu. Yeye anawasiliana na Mungu. Na kile anachotaka; ana mtoto mchanga aliye na ugonjwa wa moyo. Na huyo mtoto mchanga ana manung'uniko moyoni mwake, kwa hiyo daktari alisema. Na jina la mtu huyo ni Bw. Cox. Simama, Bw. Cox. "Naye akamwambia Sara yale aliyokuwa akiwazia, nyuma Yake."

[Ndugu Branham anaendelea kuweka mgongo wake kwa kusanyiko — Mh.]

Mle upande mwingine wa marefu ya kanisa, nyuma kidogo, kuna mtu asiye mwenyeji wa hapa, bali anatoka New Mexico. Sijapata kumwona, maishani mwangu. Ninamtazama moja kwa moja sasa, naye yuko nyuma yangu. Ametoka New Mexico. Na mtu huyo ana msichana anayependezwa naye, na msichana huyo ana kasoro kinywani mwake. Ni ... Kaa la kinywa chake ndilo baya. Na jina la mtu huyo ni Bw. West. Ungeweza kusimama, bwana. Mimi si mgeni kabisa kwake, lakini Bwana Mungu atamponya mtoto wake.

78 Je! Unaamini sasa kwa moyo wako wote? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Ni wangapi wenu wanaoamini sasa kwa moyo wenu wote? ["Amina."] Sasa, si Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele? ["Amina."] Unamkubali sasa kama Mwokozi wako? Inua mkono wako. ["Amina."] Je! Unamwamini kama mponyaji wako? ["Amina."]

Hapa, hapa kuna mtu anayeketi hapa, kiwete ama kitu fulani, amelala kwenye machela.

Unaweza kunisikia kupitia maikrofoni hii? [Ndugu Branham anachukua maikrofoni na anatembea kuelekea ukingoni mwa jukwaa na kuzungumza na mwanamke aliyekuwa kwenye machela — Mh.] Sikujui. Wewe ni mwanamke tu uliyelala pale. Kama ningeweza kukuponya, ningefanya hivyo. Siwezi kukuponya.

[Mtu anaanza kulia — Mh.] Vema. Ni mtu tu anayeshangilia. Mtoto wake aliponywa.

Sikujui. Wewe ni mwanamke, nami ni mwanamume. Hii ndiyo mara ya kwanza tumekutana maishani, nadhani. Watu hawa ...?... Waliokuleta. Kwa kweli, hii ni mara yenu ya kwanza hapa; wamekuleta tu ndani. Unatoka mbali. Umetiwa uvuli wa mauti. Una kansa. Si kiwete. Ni kansa. Madaktari hawawezi kukusaidia tena. Ni kweli. Nawe hakika utakufa; madaktari hao hawawezi kukusaidia tena.

Wakati mmoja kulikuwako na wenye ukoma watatu kwenye lango la Samaria. Na hao wenye ukoma wakasema, "Kwa nini tunaketi hapa mpaka tutakapokufa?" Kwa sababu, magonjwa yote, kufa kwa njaa, na kula watoto wao kwa wao. Walisema, "Kama tukishuka kwenda kwenye kambi ya adui, Waashuri; kama wakituua, tutakufa, hata hivyo. Na wakituokoa, tutaishi." Nao wakachukua nafasi hiyo. Na, kwa imani hiyo, hawakujiokea wenyewe tu bali kundi lote.

Sasa, utakufa kama ukilala pale. Lakini hujaombwa kwenda kwenye kambi ya adui. Lakini wewe umealikwa katika nyumba ya Baba, ...?

79 Unakufa kwa kansa. Huwezi kuishi nje ya Mungu. Wewe hutoki katika mji huu. Wewe hutoki hapa.

Umetoka mbali. Umetoka Milwaukee. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Niliuona mji huo. Ninajua jambo hilo. Hiyo ni kweli.

Unaamini? Je! Utamkubali Mungu sasa kama Mponya wako? Iwapo utafanya hivyo, haijalishi u mnyonge vipi, ulivyolemewa kitandani, naamini ningalikuwa mahali pako ningaliinuka katika jina la Yesu Kristo Na uchukue kitanda hicho na uende nyumbani, na uishi kwa utukufu wa Mungu. Je! Mtanitii, kama nabii wa Mungu? Kisha inuka uende zako. Kuwa mzima! Usiogope. Ondoka kwenye kitanda; Mungu atakuponya. Mnaona?

Mtu fulani amshikilie ili aweze kuamka na kupata nguvu. Unamwamini Mungu? Mwache tu apate nguvu kidogo; atakuwa mzima. Naam, dada. Huyo hapo, katika Jina la Bwana Yesu! [Kusanyiko linashangilia wakati yule dada sasa amesimama — Mh.]

Hebu na tusimame na kumtukuza Mungu. Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele! [Kusanyiko linashangilia sana na kumsifu Mungu — Mh.]

Nenda zako, na Bwana Yesu Kristo akubariki. [Kusanyiko linaendelea kushangilia sana na kumsifu Mungu — Mh.]



www.messagehub.info

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7